

**MBINU YA UBUNILIZI WA KISAYANSI KATIKA
RIWAYA: *Bina-Adamu* (K. W. WAMITILA) NA *Babu
Alipofufuka* (S. A. MOHAMED)**

Franklin Mukembu Mucee

Shahada ya Uzamili, Idara ya Kiswahili, Chuo Kikuu cha Kenyatta, Kenya

Prof. G. K. King'ei

Idara ya Kiswahili, Chuo Kikuu Cha Kenyatta, Kenya

Dr. R. M. Wafula

Idara ya Kiswahili, Chuo Kikuu Cha Kenyatta, Kenya

©2018

**International Academic Journal of Social Sciences and Education (IAJSSE) | ISSN
2518-2412**

Received: 15th November 2018

Accepted: 21st November 2018

Full Length Research

Available Online at:

http://www.iajournals.org/articles/iajsse_si1_1_38.pdf

Citation: Mucee, F. M., King'ei, G. K. & Wafula, R. M. (2018). Mbinu ya ubunilizi wa kisayansi katika riwaya: *Bina-Adamu* (K. W. Wamitila) na *Babu Alipofufuka* (S. A. Mohamed). *International Academic Journal of Social Sciences and Education*, 1, 1-38

IKISIRI

Utafiti huu ulihusu mbinu ya Ubunilizi wa Kisayansi katika mtindo wa riwaya teule za *Bina Adamu* K. W. Wamitila (2002) na ile ya *Babu Alipofufuka* ya S.A. Mohamed (2001). Utafiti huu hivyo basi umeonyesha kwamba sayansi bunilizi ni kipera cha riwaya kinachopatikana katika fasihi ya Kiswahili na ambacho kinaendeleza maudhui ya sayansi na teknolojia katika utamaduni wa jamii zinazotumia lugha ya Kiswahili kuwasiliana. Malengo ya utafiti huu yalijikita katika kubainisha maana ya sayansi bunilizi na kudhihirisha sifa za sayansi bunilizi zinazopatikana katika riwaya hizi. Vile vile utafiti huu ulilenga kudhihirisha-kwamba riwaya hizi zinashughulikia sayansi bunilizi mbali na kuonyesha mbinu za kimasimulizi zinazozifanya riwaya za *Babu Alipofufuka* na *Bina-Adamu* kuwa sayansi bunilizi. Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya sayansi bunilizi ambayo imehusishwa na mawazo yake Jules Verne na H.G. Wells (1950), nadharia inayoshikilia maudhui ya sayansi na teknolojia ya wakati uliopo na wakati ujao, mtindo wa kinjozi ambapo matukio ya kiajabu yanahusishwa na usimulizi usioaminika katika misingi ya uhalisia. Nadharia hii pia haionyeshi mahali na nyakati, zinaweza kuwa ni zijazo. Aidha hushughulikia maswala ya athari za sayansi na teknolojia dhidi ya maadili ya jamii. Iki kufanikisha utafiti huu data yote iliyohitajika ilikusanywa kutoka maktabani ambapo maktaba nyingi zilitembelewa kwa lengo la kukusanya data iliyohusiana na yale

yaliyoandikwa kuhusu mada ya utafiti. Mtafiti alidurusu yaliyoandikwa kuhusu sayansi bunilizi katika riwaya teule. Majarida, majuzuu, tasnifu na machapisho mengine yanayohusiana na kuafiki mada na malengo ya utafiti yalipekuliwa. Riwaya teule ambazo ni *Bina-Adamu* (2002) na *Babu Alipofufuka* (2001) zilisomwa na kuchambuliwa kwa kina ili kubainisha malengo ya utafiti yanayozifanya riwaya hizi kuwa sayansi bunilizi. Data iliyopatikana kwenye riwaya hizi ilichanganuliwa kwa kunukuliwa kwenye daftari kwa kuzingatia malengo ya utafiti kisha baadaye data hii ikawasilishwa kwa njia ya maelezo yaliyozingatia ufafanuzi wa sayansi bunilizi kama kipera cha fasihi ya Kiswahili katika riwaya. Uwasilishaji wa data ulijifunga katika malengo ya utafiti pamoja na mihimili ya nadharia teule ya sayansi bunilizi. Utafiti huu umekuwa na mchango mkubwa kwa kuwa mada ya sayansi bunilizi katika fasihi ya Kiswahili imebainisha uwiano kati ya maendeleo ya sayansi na teknolojia na sayansi bunilizi ya Kiswahili katika eneo la Afrika Mashariki. Kwa kuwa sayansi bunilizi huzungumzia mambo ya kiajabu na mapya, imeweza kuzua msamiati mpya ambao utaingizwa katika lugha ya Kiswahili na hivyo kupanua msamiati wa lugha ya Kiswahili kwa jumla. Huu ni mchango chanya kwani lugha ya Kiswahili ingali inakua.

Majina Muhimu: mbinu ya ubunilizi, kisayansi, riwaya, *Bina-Adamu*, K. W. Wamitila, *Babu Alipofufuka*, S. A. Mohamed

SURA YA KWANZA

Sura hii inahusu mada ya utafiti. Tumbainisha mada ya utafiti ambayo ni kuchunguza mbinu ya ubunilizi wa kisayansi katika mtindo wa riwaya teule za S.A. Mohamed *Babu Alipofufuka* (2001) na K.W. Wamitila *Bina-Adamu* (2002). Aidha tumeshughulikia maswala pamoja na malengo ya utafiti. Sababu za kuichagua mada ya utafiti zimebainishwa zikiwa ni pamoja na ukweli kwamba sayansi na teknolojia huathiri jamii. Mabadiliko huathiri jamii pamoja na utamaduni wake moja kwa moja. Sababu hii iliweka sayansi bunilizi katika hali ya kataka kuchunguzwa.

Katika sura hii vile vile tulijadili yaliyoandikwa kuhusu mada yetu. Kazi mbalimbali za kihakiki kuhusu sayansi bunilizi katika maandishi ya vitengo mbalimbali vya kihakiki kuhusu bunilizi mbalimbali ulimwenguni kwa jumla, barani Afrika kwenye fasihi ya Kiswahili na hatimaye katika riwaya hizi mbili zilizofanyiwa utafiti. Upeo na mipaka ya utafiti pia ilishughulikiwa katika sura hii na hatimaye nadharia tuliyoitumia imeelezwa. Mwisho tuliangaza muundo wa utafiti, mahala pa utafiti, uteuzi wa sampuli, uchanganuzi wa data na uwasilishaji wa data.

Usuli wa Mada ya Utafiti

Kwa majibu wa Richard katika Wikipedia sayansi bunilizi ni fasihi ya mabadiliko. Utamaduni unapitia mabadiliko mengi kutokana na maendeleo ya sayansi na teknolojia. Sayansi bunilizi kwa hivyo hueleza athari za sayansi na teknolojia kwa wanajamii. Hadithi kuhusu mabadiliko haya zimekuwa maarufu kama njia za kueleza matamano, hisia na mielekeo kuhusu mabadiliko. Mabadiliko haya yanaweza kuwa katika uwezo wetu wa kuudhibiti ulimwengu ama kuuelewa. Kwa mfano, baadhi ya hadithi za awali kama “kuzaliwa upya” huonyesha tamaduni zinazoeleza na kudhibiti ulimwengu kwa kiasi kidogo kuliko tamaduni za leo. Elementi za kisayansi husheheni uelewa wetu wa ulimwengu ‘wao’ na jinsi ulivyoibuka kutoka ulimwengu wetu. Hadithi zingine hutupa teknolojia zitakazokuja, ambazo tunaweza kutegemea kutokana na sayansi ya leo lakini haijakuwa bado mathalan roketi za kinuklia.

Tunaweza kuamini kuwa ulimwengu unaorejelewa kwenye hadithi waweza kuwa katika siku zijazo. Kuna aina ya sayansi bunilizi iliyo burudani tupu. Katika utangulizi wa riwaya ya Isaac Asimov (1955), hadithi ya sayansi bunilizi lazima idhihirishe mandhari ya jamii yaliyo tofauti kabisa na jamii yetu kwa sababu ya mabadiliko katika kiwango cha sayansi na teknolojia. Hadithi za sayansi bunilizi hugaribu utulivu kwa kuvuruga michakato ya kufikiria katika jamii na huwa hazijihusishi na kurejesha amani katika jamii bali mabadiliko; yanayoendelea kutokea. Kama nilivyotanguliza kusema, sayansi bunilizi ni fasihi ya mabadiliko, mabadiliko ndicho kitu cha kudumu na kwa vile sayansi bunilizi huhusisha maudhui mapana katika jamii na tanzu ambazo ni muhali kufafanua. Sayansi bunilizi imehakikiwa katika sehemu nyingi ulimwenguni.

Imeshughulikiwa huko Uingereza na Marekani kwa mapana na marefu. Katika miaka ya 1990, kulikuwepo na filamu mashuhuri zilizoitwa *Star Wars* huko Marekani. Lengo kuu la filamu hizi lilikuwa kuonyesha viumbe wa ajabu walioishi katika sayari nyinginezo. Tahakiki za sayansi

bunilizi za kimagharibi pia ni nyingi. Hata hivyo, kwa maoni yangu uhakiki unaotilia maanani sayansi bunilizi kwa kurejelea fasihi ya Kiswahili haujafanyiwa utafiti mpana na wa kina. Hii sababu imetufanya kushughulikia mada hii.

SWALA LA UTAFITI

Utafiti huu ulishughulikia mbinu ya ubunilizi wa kisayansi katika mtindo wa riwaya teule. Sayansi bunilizi ni fasihi ya mabadiliko. Utamaduni unapitia mabadiliko mengi kutokana na maendeleo ya sayansi na teknolojia (Richard Wikipedia). Vile vile sayansi bunilizi ni kiungo muhimu cha fasihi kwani hadithi na tungo kuhusu mabadiliko zimekuwa maarufu kama njia za kuelezea hisia na mielekeo kuhusu mabadiliko. Utafiti huu ulibainisha na kuchanganua vipengele mbalimbali vya sayansi bunilizi katika riwaya za Bina-Adamu K.W. Wamitila (2002) na ile ya Babu Alipofufuka S.A. Mohamend (2001). Kwa kufanya hivyo utafiti huu ulionyesha kwamba sayansi bunilizi ni kipera cha riwaya kinachopatikana katika fasihi ya Kiswahili na ambacho kinaweza kuendeleza maudhui ya sayansi na teknolojia katika utamaduni wa jamii zinazotumia lugha ya Kiswahili kuwasiliana.

MALENGO YA UTAFITI

1. Kuadhihirisha sifa za sayansi bunilizi zinazopatikana katika riwaya teule.
2. Kubainisha maudhui katika riwaya hizi yanayodhihirisha kuwa zinashughulika na sayansi bunilizi.
3. Kudhihirisha mbinu za kimasimulizi zinazozifanya riwaya za Babu Alipofufuka na Bina-Adamu kuwa ni za sayansi bunilizi.

SURA YA PILI

Historia ya sayansi bunilizi katika misingi ya kimagharibi na fasihi ya Kiswahili

Kwa mujibu wa *American People's Encyclopedia*, sayansi bunilizi ni kipera cha kipekee kilicho na historia ya kutoka karne ya kumi na tisa na kinahusishwa na Plato, Lucian, Francis Bacon, Bishop Francis, Godwin, Johannes Kepler, Jonathan Swift, Sir Thomas More, Lewis Holberg na Edgar Allan Poe.

Poe aliifanya sayansi bunilizi kuwa ya filozofia na yenye utafiti wa kindani zaidi. Jules Verne aliweka ruwaza ya sayansi bunilizi ya kisasa ikiwemo fasihi ya Kiswahili hasa kipera cha riwaya ambapo utafiti huu unajikita; aidha ilijikita katika dhana za kisayansi na utabiri jambo lililopelekea baadhi ya waandishi kuirejelea kama fasihi ya 'kinabii'. Wells alipiga hatua kwa kuweka vigezo vya kifilosofia vya sayansi bunilizi.

Mwaka wa 1939 jumba la Arkham lilijengwa na ndipo kitabu cha mwandishi Alfred Elton Van Vogt kilichojulikana kama *Slan* kilichapishwa. Uchapishaji wa kitabu hicho ulichochea uchapishaji wa sayansi bunilizi katika vitabu kamili na vyenye jalada gumu badala ya majarida.

Miongoni mwa majarida ya sayansi bunilizi katika miaka ya 1960 ni *The Magazine of Fantasy and Science Fiction* kilichoandikwa haririwa na Anthony Boucher; *Astounding Science Fiction* nacho kikahaririwa na John W. Campbell Jr. Wahariri hawa ndio waliowaongoza waandishi wa sayansi bunilizi katika mitindo mipya.

Kutoka mwanzoni mwa 1920 wafuasi wa sayansi bunilizi waliojitolea zaidi walibuni kazi fupi na za muda zilizojulikana kama *Fanzies* zilizowafanya kuwa makini kuhusu hadithi, waandishi, muelekeo na uvumbuzi mpya wa kisayansi miongoni mwa maswala mengine kuhusu sayansi bunilizi. Makongamano ya kila mwaka yalipangwa Marekani na kwingineko, shughuli iliyosisitizwa na wafuasi wa sayansi bunilizi wa kujitolea. Kwa kuwa uhakiki mwingi wa sayansi bunilizi unatokana na fasihi ya kimagharibi, katika utafiti huu tumetegemea historia ya sayansi bunilizi ya kimagharibi ili kujenga misingi thabiti ya uhakiki wa sayansi bunilizi katika Kiswahili.

Sayansi bunilizi katika karne ya kumi na tisa ya Magharibi na Afrika

Sayansi bunilizi ina kiini chake katika filozofia ya Kirumi ya karne ya kumi na tisa. Kwani fasihi ya karne ya kumi na tisa ilichochea na filozofia hii ambayo ilisisitiza hisia na ari ya kibinadamu ya kuisoma sayansi bunilizi. Katika karne ya kumi na tisa hadithi zilizoandikwa zilikuwa za kiajabu na za kutisha ambapo hadithi za kilimbwende zilikuwa maarufu sana. Hadithi hizi zilikuwa na lengo la kutekenya na kuibua hisia hasi au chanya za wasomaji. Sayansi bunilizi inavyo vipindi maalum ambavyo ilipita kutoka mwanzo hadi kufikia kiwango ilichoko hivi leo. Baadhi ya vipindi hivi ni kama vile, kipindi cha kilimbwende, kipindi cha kiwewe, kipindi cha mafanikio makuu, kipindi cha almasi cha sayansi bunilizi, kipindi cha wanawake na kile cha milenia mpya. Utunzi wa kisayansi bunilizi husisitiza uhalisia kwa njia ya uwazi na isiyoibua hisia.

Sayansi bunilizi ya karne ya kumi na tisa ilijulikana kama sayansi ya kilimbwende (scientific romances). Kwa mujibu wa Robert Hoskins, Edgar Allan Poe (1809-1849) ndiye alikuwa mwandishi wa kwanza wa karne hiyo aliyehusisha vipengele vya kilimbwende na kisayansi katika hadithi zake. Alikuwa mwandishi wa hadithi kongwe zaidi na vilevile mpya zaidi. Hadithi yake kongwe zaidi ilijulikana kama *Hoax* na ililenga kujenga mtandao wa kusambaza uchapishaji wa gazeti. Hata hivyo hadithi hiyo, ilisheheni ufafanuzi wa kisayansi uliopangika kimantiki kiasi cha kwamba hata wahandisi wa roketi za anga hawangezipinga. *The Balloon-Hoax* ni mfano wa hadithi aliyoiandika Poe iliyohusu habari za kuisimua kama vile, *The Atlantic Crossed in Three Days*. Wahakiki wengine wa hadithi hizi za Poe ni Mr. Monck na mhakiki aliandika hadithi *Signal Triumph*, Mr. Mason na hadithi yake *Mason's Flying Machine Arrival at Sullivans Island near Charleston*. Mr. Henson, Harrison Ainsworth pia ni wahakiki wake Poe.

Thomas Disch anadai kwamba Poe ndiye mwasisi wa sayansi bunilizi ya kisasa. Poe anajulikana kwa hadithi zake za kutisha za kiungu, lakini alijumlisha mawazo na makisio ya kisayansi ili

kuleta athari za kisaikolojia katika hadithi zake. Mkondo wa kilimbwende katika sayansi bunilizi hutia motisha mbali na kutisha na kuhofisha wasomaji.

Kuna uhusiano kati ya sayansi na sayansi bunilizi. Sayansi iliathiri usimulizi wa hadithi katika kipindi cha kisasa na kuhusishwa huku kuliibua sayansi bunilizi. John Clute katika kazi ya kibunilizi *'The illustrated Encyclopedia'* ameeleza historia ya sayansi bunilizi kwa kutoa fasiri ya hali bainifu ya sayansi bunilizi. Clute anaeleza kuwa enzi za kale watu waliandika Fantasia kuhusu safari za anga za juu ambapo walipatana na viumbe vya kutisha kiajabu. Kwa mujibu wa Clute waandishi wa hadithi za awali hawakufafanua iwapo matukio waliyozungumzia katika hadithi zao yangetokea katika hali halisi za kimaisha.

Clute alitetea kauli kwamba fantasia za kabla ya usasa zingekuwa uhalisia tu baada ya mapinduzi ya kisayansi katika kipindi cha usasa. Clute alidai kwamba kazi yake Moore iitwayo *"Utopia"* (1516) na iliyoandikwa kabla ya kipindi cha usasa haikukusudiwa kuleta uhalisia. Kazi yake Francis Bacon's *The New Atlantis* (1626) ilikusudiwa kuwa ya uhalisia. Bacon aliweka msingi wa kutabiri uvumbuzi mpya na uhalisia wa wakati ujao kupitia mawazo ya Kisayansi.

Johannes Kepler ni mwandishi mwingine wa sayansi bunilizi ya awali *Somium seu Astronomia Lunari* (1634). Kwa mujibu wa Wyn Wachhorst akinukuliwa katika *Somium*, Kepler alikuwa wa kwanza kuandika sayansi bunilizi kuhusu safari ya kwenda mwezini na vilevile akawa wa kwanza kudai uwezekano wa kuishi katika sayari nyingine. Kwa mujibu wa Clute asili ya sayansi bunilizi ilisadifu na kuchipuka kwa wazo la maendeleo na mabadiliko katika wakati ujao kutokana na sayansi.

Madai ya Clute ni kuwa sayansi bunilizi ya wakati ujao iliibuka wakati matumaini na utabiri wa maendeleo yalikusishwa katika usimulizi wa hadithi katika sayansi bunilizi, mambo yaligeuka kinyume na kwa hivyo sayansi, maendeleo ya nchi, pamoja na maendeleo ya kiteknolojia yanaweza kutuamamiza. Kazi yake Mary Shelley (1797-1851) ya karne ya kumi na tisa ilitabiri uwezekano wa hatari ya sayansi na teknolojia.

Karne nzima ya kumi na tisa kulikuwa na hadithi zenye mielekeo chanya yenye matumaini kutokana na teknolojia, maendeleo ya dunia na nchi inayopendeza. Matumaini haya yalifululiza na kukaandikwa vitabu kama vile kitabu chake Samuel Butler *Erewhon* (1872) na kitabu chake Edward Bellamy *Looking Backward* (1888). Kwa mujibu wa Laura Lee, katika miaka ya 1888-1900 riwaya 150 ziliandikwa lakini kinadharia ploti yazo ilijikita katika mwaka wa 2000. Msomaji anarejeshwa kutoka mwaka 1888 na kupelekwa hadi mji wa Boston mwaka wa 2000 kupitia maendeleo ya kiteknolojia. Kutoka mwanzo, sayansi bunilizi huhusisha hadithi chanya za kumotisha na vilevile za kuhofisha. Sayansi bunilizi humtayarisha msomaji kwa mazuri na mabaya yanayotokana na maendeleo ya sayansi na teknolojia.

Kwa mujibu wa Brian Aldiss waandishi Jules Verne (1828-1905) na H.G Well (1866-1946) ndio walioifanya sayansi bunilizi kuwa maarufu mwishoni mwa karne ya kumi na tisa. Na kwa

mara ya kwanza sayansi bunilizi ikawa na athari kubwa katika utamaduni maarufu katika kazi za waandishi hawa wawili. Jules Verne ndiye maarufu katika utabiri wake wa kiteknolojia na uvumbuzi wa mambo mapya. Haya yanadhihirika katika kazi yake ya mwaka wa (1883) *Around the world in Eighty Days* na vile vile katika kazi yake *A Journey to the Center of the Earth* (1864), aliandika kazi nyingine katika mwaka wa 1865 *From the Earth to the Moon*. Riwaya za Jules Verne ziliweka msingi wa dhana ya maendeleo ya dunia kupitia maendeleo ya sayansi na teknolojia. H.G. Wells aliweka pamoja mawazo ya kijamii, kihistoria na filofia katika mtazamo wa sayansi na teknolojia. Wells aliandika kazi nyingi za kibunilizi, kimasimulizi na vile vile zisizo za kibunilizi kuhusu wakati ujao/baadaye.

Herbert George Wells ndiye baba wa sayansi bunilizi ya kisasa. Mwandishi wa kibunilizi Thomas Disch anamtaja Wells kuwa mwandishi maarufu miongoni mwa waandishi wote wa kibunilizi. Kazi alizoandika ni pamoja na, *The Time Machine* (1895), *The Island of Dr. Moreau* (1896), *The Invisible man* (1897), *The war of the world's* (1898) na “*When the Sleeper Awakes*” (1899). Kazi nyingine ni pamoja na *The first men in the Moon* (1901), *The Food of the Gods* (1904), *The war in the Air* (1908), *The World set Free* (1914) na *The Shape of Things to Come* (1933). Kwa mfano H.G. Wells aliandika hadithi, *The Time Machine* ya Kidaikronia iliyokuwa ya kuogofya na kutisha. Hadithi hii ni ya kutahadharisha kwamba tusipobadilisha jamii na jinsi tunavyofikiria pamoja na matendo yetu tutajikuta taabani. Hadithi hii inahusu ulimwengu wa baadaye ambapo binadamu hasa mabwenyenye na wafanyikazi wameibuka na wakajiweka katika matabaka mawili walalahai na walalahoi.

Walalahoi hufanya kazi zote za sulubu viwandani na kuwalisha walalahai ambao huishi maisha ya kitoto katika miji ya starehe inayotunzwa na walalahoi. Kwa kifupi hadithi hii inawaweka wanajamii katika matabaka mawili, tabaka la juu na tabaka la chini. Wanajamii wa tabaka la chini hufanya kazi zote za sulubu na kuwalisha matajiri wa tabaka la juu ambao kazi yao ni kustarehe.

Wells pia aliandika msururu wa kazi za filofia kuhusu wakati ujao. Kazi ambazo ni pamoja na *The Discovery of the Future* (1902), *Anticipations of the Reaction of Mechanical and Scientific Progress upon Human Life and Thought* (1902), *Mankind in the Making* (1903) *The Open Conspiracy: Blue Prints for a World Revolution* (1928) *World Brain* (1938) *The Fate of Homo Sapeins* (1939) na *Mind at the End of its Tether* (1945).

Wells alipendelea kukisia uwezekano wa matukio ya baadaye ya binadamu. Wells alitabiri mambo mengi ya baadaye kama vile mabomu ya atomiki, nguvu za kinuklia vita vya angani, mitandao ya utangazaji, miongoni mwa mengine. Baadhi ya haya yamekwisha timia ikiwa ni pamoja na vita vya dunia.

Sayansi bunilizi ya mwongo wa kwanza wa karne ya ishirini katika Magharibi na Afrika

Clute anarejelea kipindi cha mwongo wa kwanza wa karne ya ishirini kama *A Glowing Future* kwani ufanisi ulikua haraka na uvumbuzi ulikuwa kila mahali, ikiwemo Afrika hasa Afrika Mashariki. Kulikuwa na matumaini upande wa Magharibi kwani ustaarabu, sayansi na teknolojia ziliendelea wakati huu. Pia kulikuwa na matukio mengi katika sayansi, sanaa na utamaduni. Riwaya nyingi kuhusu vita vya baadaye ziliandikwa ikiwa ni pamoja na riwaya yake Wells *The War in the Air* na katika fasihi ya Kiswahili riwaya ya *Bina-Adamu* inayo maudhui ya vita vya baadaye. Katika mwongo kabla ya vita vya kwanza vya dunia kulikuwa na mizozo iliyovuruga akili za watu na changamoto kuhusu uhalisia. Hili ni jambo alilozungumzia Wells.

Clute anaamini kuwa hadithi za kibunilizi kuhusu wakati ujao ziliandikwa kama tahadhari za mikasa. Katika mwongo wa pili wa karne ya ishirini sayansi bunilizi ilipiga hatua kutokana na vitisho vya vita vya dunia. Wakati huu mwandishi Edgar Rice Burroughs (1875-1950) alianzisha kazi zake maarufu kama *Barsoom* kuhusu watu wa Mars *and na ustaarabu wao* pamoja na *Under the Moon of Mars* (1912). Burroughs alibuni *msururu wa* riwaya iliyojulikana kama *The Land that Time Forgot* (1924).

Kazi zake zilikuwa maarufu kupitia utafiti wake wa kulisimua. Katika kipindi hiki kazi nyingi ziliandikwa kuhusu falme pamoja na roketi za angani. Katika miaka ya ishirini (1920) kupitia msisimko wa Hugo Gernsback dhana sayansi bunilizi iligeuka kuwa maarufu sana na kutumika zaidi. Neno hili liliibuka kutokana na usayansishaji kupitia kwa Gernsback.

Gernsback alitumia sayansi bunilizi kufafanua aina za hadithi alizochapisha kama mhariri mwasisi katika jarida lake lililoitwa '*Amazing Stories*' kuanzia mwaka wa 1926. Gernback alikuwa mwandishi mchangamfu sana kuhusu maajabu na umuhimu wa teknolojia ya wakati ujao. Gernsback alichochewa na kazi zao Wells na Jules Verne miongoni mwa wengine, ndipo akaanzisha msururu wa majarida mapya *Amazing stories Science Wonder stories, Air Wonder Stories* na *Amazing stories Quarterly* yote yakiwa na lengo la kudhihirisha vile sayansi na teknolojia ingebadilisha dunia kuwa na teknolojia ya kiutopia. Mnamo mwaka wa 1926 kuliibuka filamu kwa jina 'Metropolis' ambayo ilionyesha maendeleo ya kiteknolojia.

Katika miaka ya ishirini vile vile roboti zilikuwa maarufu sana katika sayansi bunilizi. Jina roboti linatokana na tamthilia ya Karel Capek iliyoitwa Rossums *Universal Robots* mwaka wa 1924. Katika sayansi bunilizi inahofiwa kuwa roboti hutengenezwa na binadamu lakini huenda likawageuka baadaye na kuwaangamiza.

Katika miaka ya kwanza ya sayansi bunilizi roboti zilifanana na binadamu. Roboti na tabia zake zilifanana na za binadamu. Roboti katika sayansi bunilizi ziliibuka kuwa ishara ya binadamu kuwa kama mashine kutokana na matumizi mengi ya mashine. Kwa kurejelea riwaya hizi teule za *Bina-Adamu* na *Babu-Alipofufuka* kwa kuwa na sifa bainifu za sayansi bunilizi ni kipera cha

riwaya katika fasihi ya Kiswahili na kinaendeleza maudhui ya sayansi na teknolojia katika utamaduni wa jamii zinazotumia ligha ya Kiswahili kuwasiliana.

Kipindi cha mafanikio makuu cha sayansi bunilizi ya Magharibi na Afrika

Katika miaka ya 1930 na 1940 sayansi bunilizi ilikua na kupata umaarufu zaidi kule Magharibi na kwingineko Afrika ikiwemo. Kipindi hiki kinajulikana kama kipindi cha mafanikio makuu cha sayansi bunilizi. Majarida ya sayansi bunilizi yalichipuka na waandishi wengi wapya walijitosa katika uandishi wa majarida hayo akiwemo mwandishi maarufu Isaac Asimov na Robert Heinlein. Isaac Asimov na Robert Heinlein walianza kuchapisha hadithi fupi mnamo mwaka wa 1940. Asimov alibuni msururu wa hadithi za roboti ambazo alikuwa maarufu kwazo. Heinlein naye aliziweka hadithi zake pamoja na akaibuka na historia ya baadaye ya jamii iliyoopenya karne kadha baadaye. Baadaye Asimov aliibuka na historia ya wakati ujao maarufu kama '*Foundation Series*'.

Flash Gordon alijitokeza katika magazeti na baadaye akatoa filamu za video. Sayansi bunilizi ilipata umaarufu kupitia vyombo vya habari kama vile redio na kanda za video. Kwa mfano Orson Wells alipeperusha kipindi cha *The War of the World's* kipindi ambacho kilihofisha mamilioni ya watu kote Amerika. Filamu za *Frankenstein*, *The Invisible Man* na *Dr. Jekyll* na *Mr. Hyde* zilitolewa katika kipindi hiki.

Aina ya sayansi bunilizi iliyovuma katika kipindi cha Mafanikio Makuu ilikuwa the *Space Opera*. Hii ni michezo ya kuigiza ya kiepiki inayohusisha utafiti na hatari na zana za vita za kiteknolojia. Katika kipindi hiki E.E Smith aliongoza katika kukuza na kuifanya *Space Opera* na aliandika riwaya mbili maarufu zilizojulikana kama *The Skylark of space* na *Lensmen*.

Mwana filofia wa Uingereza Olaf Stapledon (1886-1950) ambaye aliandika miaka ya 1930 ndiye maarufu zaidi miongoni mwa waandishi wote wa sayansi bunilizi. Vilevile Stapledon ndiye mwandishi mbunifu zaidi katika historia ya sayansi bunilizi. Stapledon aliandika riwaya tano pekee za sayansi bunilizi. Mnamo mwaka wa 1930 Stapledon aliandika riwaya mbili za kiepiki za kusisimua za wakati ujao wa mbali. Riwaya ya kwanza ikiitwa '*Last and First Men*' (1930) ambayo ilirejelea historia ya binadamu katika miaka billion mbili ijayo na ile ya pili ikiitwa *Star Maker* (1937). Arthur C. Clarke (2001) anaeleza riwaya ya *Star Maker* kama kazi ya ubunifu wa kipekee kuwahi kuandikwa kwa kuwa inatalii dhana ya miaka ya mbali sana ya baadaye, yaani bilioni kadha kutoka sasa. Clarke aidha anadai kwamba hadithi hii ni kisasili kikuu cha wakati ujao. Hii ni sawa na ilivyo katika baadhi ya riwaya za Kiswahili kama vile *Bina-Adamu* riwaya inayosimulia kisasili cha chanzo cha kijiji chao.

Waandishi Isaac Asimov na Robert Heinlein walikuwa maarufu katika kipindi cha Mafanikio Makuu (*Golden Age*) cha sayansi bunilizi; waliendelea kuandika riwaya nyingi maarufu kwa miongo kadhaa hadi miaka ya 1960 na 1970. Waandishi hawa walianza kuchapisha hadithi fupi mnamo mwaka wa 1940 ambapo Asimov aliandika hadithi nyingi za roboti. Heinlein kwa

upande mwingine alikuwa maarufu kwa kuunganisha hadithi zake zilizoeleza historia ya jamii za wakati ujao. Sawa na waandishi wa Afrika kama vile S.A Mohamed katika *Babu-Alipofufuka* na K.W.Wamitila katika *Bina-Adamu* ambao walieleza historia za jamii.

Asimov vile vile alibuni historia yake ya baadaye ambayo ilikuja kujulikana kama ‘*Foundation Series*’. Hadithi zao Asimov na Heinlein zilihusisha utabiri wa teknolojia, safari za angani na ukoloni. Waandishi hawa walichochea mawazo ya kisaikolojia, sosholojia na kihistoria ambayo yaliwapelekea kubuni historia ya maendeleo ya binadamu. Asimov aliangazia mabadiliko ya kihistoria na athari zinazoathiri mabadiliko ya jamii naye Heinlein akijihusisha na maswala ya siasa, dini na mielekeo ya jamii kwa jumla. Kufikia mwaka wa 1940 sayansi bunilizi ilikuwa imepiga hatua katika mambo ya uchunguzi wa jamii, siasa, teknolojia na matukio ya baadaye. Asimov pamoja na Heinlein waliongoza katika kuchunguza na kuvumbua kuwepo kwa jamii na siasa ya kesho.

Katika hadithi za roboti za Asimov aligusia hofu ya binadamu ya uvumbuzi wa teknolojia na kwa hivyo aliibuka na maelezo ya jinsi ya kutengeneza mashine ambazo hazingemdhuru binadamu, Katika harakati hii Asimov alibuni: ‘*The Three Laws of Robotics*’ (sheria tatu za roboti). Hizi zinapatikana katika mkusanyiko wa hadithi zake. Mbali na Asimov na Heinlein kulikuwa na waandishi wengine maarufu waliochipuka katika kipindi cha Mafanikio Makuu (*Golden Age*) waandishi hawa ni Ben Boras aliyeandika hadithi *The Science Fiction Hall of Fame* na Raymond Healy na J. Francis McComas ambao waliandika *Adventures in Time and Space*.

The Science Fiction Hall of Fame ni mkusanyiko wa hadithi fupi na novela, mkusanyiko ambao uliteuliwa kuwa bora zaidi na wanachama wa *Science Fiction Writers of America*. Asili mia kubwa ya vitabu katika mkusanyiko huu vimetokana na kipindi cha Mafanikio Makubwa. Katika vitabu hivi viwili hadithi zilizomo zinahusu ustaarabu wa ughaibuni, safari za wakati, na wakati ujao pamoja na roketi za angani na haya yote ni maudhui ya sayansi bunilizi ya karne ya ishirini.

Waandishi wanaohusishwa katika mikusanyiko hii miwili ni Lewis Padgett ambalo ni jina la msimbo la Henry Kuttner na Catherine Moore hawa ndio waandishi maarufu zaidi katika historia ya sayansi bunilizi. Hawa walikuwa bwana na bibi na hadithi zao bora zaidi ni pamoja na Mimsy Were the Borogroves na Vintage Season kazi ambazo ziliandikwa katika mwaka wa 1940. Hadithi nyingine iliyoandikwa katika mwaka wa 1940 na Kuttner wakishirikiana na Moore ni *Private Eye*. Hii inapatikana katika mkusanyiko wa hadithi za kibunilizi maarufu kama ‘*The Mirror of Infinity*’ kitabu kilichohaririwa na Robert Silverberry. *Private Eye* ni sayansi bunilizi ya kisaikolojia.

Riwaya za mwaka wa 1930 na 1940 ziliangazia madhara ya maendeleo ya kiteknolojia. Riwaya hizi za Kidaistopia ni ile ya *Brave New World* iliyoandikwa na Aldous Huxley mwaka wa 1932 na ile ya pili ni *Dystopia* iliyoandikwa na George Or well 1984 mnamo mwaka wa 1949 Daistopia ni kinyume cha *Utopia*. Riwaya hizi ziliandikwa kama tahadhari dhidi ya maendeleo

ya kijamii na kisiasa ulimwenguni. Baada ya matumaini ya karne ya kumi na tisa ulimwengu mpya uliingia katika kipindi cha kuhangaika na mabadiliko. Matumaini yakayeyushwa na vita vya kwanza na vya pili vya dunia uongozi wa kiimla, kudidimia na kuzorota kwa uchumi kutupiliwa mbali kwa sayansi sanaa na filofia.

Kipindi cha kiwewe cha sayansi bunilizi katika Magharibi na Afrika

Mapema karne ya ishirini maisha ya baadaye yalianza kuhofisha na kukaingia kipindi cha shauku kuu kilichojulikana kama kipindi cha kiwewe wakati huu riwaya *Brave New World* na 1984 zilitilia hali hii nguvu zaidi na kuthibitisha hali ya ulimwengu mpya. Riwaya *Brave New World* na 1984 si sayansi bunilizi halisi kwani zinaangazia tahakiki ya jamii na tahadhari kuhusu maendeleo ya kisiasa na kisaikolojia katika muktadha wa wakati ujao. Sayansi bunilizi iliendelea sambamba na karne ya ishirini. Wakati huu waandishi wa kiafrika akiwemo Said Ahmed Mohamed aliingiwa na shauku kubwa ya kuandika riwaya kinyume na hapo awali alipokuwa akiandika hadithi fupi.

Katika muktadha wa sayansi bunilizi, yaliyoandikwa katika 1984 na *Brave New World* yalikuwa finyu sana katika kipera hiki. Hii ni kwa sababu yaliyoandikwa yalikuwa kinyume na maoni yake Gernsback ambaye alishikilia kwamba sayansi bunilizi haihusu sayansi na teknolojia ya wakati ujao bali ilipaswa kuhusu mitazamo mingi ikiwemo uhalisia wa binadamu, kama vile jamii, siasa na saikolojia.

Kipindi cha almasi cha sayansi bunilizi katika Magharibi na Afrika

Miaka ya 1950 inarejelewa kama Kipindi cha Almasi cha sayansi bunilizi (*The Silver Age of Science Fiction*) wakati huu dhana na ishara ya sayansi bunilizi iliendelea kuingia katika akili za watu wakiwemo waandishi wa kiafrika. Mzozo baina ya Marekani na muungano wa Usovieti ulipelekea utabiri wa awali kuhusu roketi za angani kutimia na kuwa halisi. Wakati huu basi kanda maarufu za filamu zilitolewa kama vile *Forbidden Planet*, *Destination Moon*, *Earth Verses the Flying Saucers*, *The Day the Earth Stood Still*, *The Thing*, *The Fly*, *Them*, *This Island Earth*, *Invasion of Thee Body Snatchers*, *Invaders from Mars*, *War of the Worlds* na *On the Beach*. Katika Afrika uhalisia ulishuhudiwa pale ambapo waandishi walijumlisha matukio hayo katika kazi zao akiwemo mwandishi K.W.Wamitila katika kazi yake *Bina Adamu*.

Kupitia filamu hizi na zingine nyingi athari ya sayansi bunilizi kwa utamaduni iliendelea kukua. Kwa mfano ni wakati huu ambapo 'Flying saucer craze' ziliibuka na zikaenea baada ya sayansi bunilizi na kuzitazama katika filamu. Matukio ya kiajabu yaliyotabiriwa katika kazi yake H.G. Wells *The War of the World* yalianzia kuwa maarufu. Baada ya mzozo na makabiliano kati ya Marekani na Muungano wa Usovieti uliopelekea kulipua mabomu ya kiatomiki mnamo mwaka wa 1945 ndipo maangamizi dhidi ya ustaarabu wa kibinadamu yalizua uhalisia uliotabiriwa na waandishi wa awali.

A Canticle for Leibowitz ni hadithi maarufu ya miaka ya hamsini iliyoandikwa na Walter Miller kuhusu vita vya kiatomiki na athari zake. Kazi hii ilishinda tuzo na wengi waliithamini kuwa riwaya maarufu sana ya sayansi bunilizi ya miaka ya hamsini. Katika miaka ya 1950 sayansi bunilizi kama kigezo cha kitamaduni na kipera cha fasihi ilikubaliwa na ikapangika kwa misingi ya kijamii.

Mnamo mwaka wa 1953 tamasha za mwaka za kutuza maarufu kama Annual Hugo Awards zilibuniwa katika *World Science Fiction Convention* (muungano wa kimataifa wa watunzi wa sayansi bunilizi). Muungano wa Hugo ulithamini riwaya, novela na hadithi fupi, filamu na ufanisi mwingine wowote bora katika nyanja ya sayansi bunilizi. Mshindi wa kwanza katika kitengo cha riwaya bora alikuwa Alfred Besters na riwaya yake maarufu *The Demolished Man* kwa mara kadhaa World Science Fiction convention iliendelea na ikawa maarufu zaidi na kuenea kote Marekani. Kwa kubuniwa kwa *World Science Fiction Convention* na tuzo ya Hugo sayansi bunilizi ilibadilika na kuwa swala la kijamii na kutambulikana kote Marekani na sehemu zingine ulimwenguni ikiwemo Afrika hasa Afrika Mashariki. Watu, waandishi, wasomi na mamilioni ya mashabiki waliienzi na kuipenda sayansi bunilizi na hivyo kusambaza maono na mawazo ya Wells, Heinlein, Asimov na Clarke.

Kwa kuwa mbinu za kimasimulizi katika riwaya ya *Bina-Adamu* na *Babu Alipofufuka* zinashabihiana na sayansi bunilizi basi huenda baadhi ya waandishi na wasomi walioenzi sayansi bunilizi ni pamoja na Wamitila na S.A Mohamed ambao ndio waandishi wa riwaya teule zilizochunguzwa.

Mwaka wa 1965 waandishi wa sayansi bunilizi na Fantasia wa Marekani waliunda tuzo za Nebula. Mashabiki wa sayansi bunilizi wa tuzo za Hugo waliupigia kura ilhali wale wa mrengo wa *Science Fiction and Fantasy Writers of America* wakapigia tuzo za Nebula kura. Kuliibuka ushindani mkubwa baina ya makundi haya mawili na hivyo kupelekea sayansi bunilizi kupiga hatua kubwa kimaendeleo. Kwa mujibu wa Clute mnamo miaka wa 1960 sayansi bunilizi ilibadilika kuwa ukweli, roketi zilianza kupaa angani kupeleleza kama ilivyokuwa imetabiriwa na Arthur C. Clarke. Mwanzoni mwa mwongo Yuri Gagarin akawa binadamu wa kwanza angani na mwishoni mwa mwongo binadamu walikuwa wametua mwezini. Hii ilikuwa ndoto na utabiri tangu enzi ya Kepler.

Clute anadai kwamba kipindi hiki kwa jumla kilihusisha mawazo mapya na matumaini kuhusu wakati/maisha ya baadaye. Vile vile hali ilirejelea wakati uliopita katika historia ya magharibi. Kulikuwa na imani chanya kuhusu teknolojia na uvumbuzi. Binadamu alikuwa na uwezo wa kuyadhibiti maisha ya baadaye. Miaka ya 1960 kwa mujibu wa Clute ilikuwa wakati wa ubunifu wa utamaduni na teknolojia pamoja na imani ya wakati ujao. Miaka ya sitini ilikuwa ya mabadiliko ya kijamii na kiteknolojia ingawa kulikuwa na uchangamano pamoja na ukosefu wa utulivu. Kulikuwa na imani na vilevile kutokuwa na imani.

Mwongo huu ulishuhudia mwanzo wa mabadiliko ya kijamii ya Magharibi mpya kinyume na mawazo ya usasa. Maadili ya zamani ya kijamii yaliathiriwa. Maendeleo ya kiuchumi na kiteknolojia yalipuuziliwa na wanajamii na kukawa na uasi wa maendeleo ya kiteknolojia na watu kutaka kurejelea hali yao ya awali kabla ya ustaarabu. Miaka ya sitini ilikuwa na ujarabati wa tamaduni kama vile mapenzi, kujitambua, uvumbuzi na uhuru. Wakati huu sayansi bunilizi ilijihusisha na maudhui ya kisaikolojia, kijamii na ubinadamu kinyume na ilivyokuwa hapo awali wakati ilipojihusisha na tahakiki ya jamii na tahadhari kuhusu matokeo hasi kutokana na maendeleo ya kiteknolojia.

Kipindi cha mwamko mpya cha sayansi bunilizi katika Magharibi na Afrika

Sayansi bunilizi katika miaka ya sitini ilishuhudia mwanzo wa Mwamko Mpya kwani majaribio ya mtazamo wa kifasihi, kisaikolojia na maandishi ya kibinadamu yalitokea kuwa maarufu sana. Katika kipindi hiki riwaya tatu maarufu zilizoshinda tuzo ya Hugo zilichapishwa zikiwa ni pamoja na *Stranger in a Strange Land* iliyoandikwa na Robert Heinlein, '*Dune*' iliyoandikwa na Frank Herbert na *The man in the High Castle* iliyoandikwa na Philip K. Dick. Riwaya hizi tatu ziligusia maudhui ya utamaduni na utabiri wa imani za kijamii na kidini. Harlan Ellison alikuwa mwandishi maarufu sana wa hadithi fupi katika kipindi hiki cha *New Wave*. Mnamo mwaka wa 1966 Ellison alishinda tuzo ya Hugo kupitia hadithi fupi kwa jina la *Repent Harlequin said the Ticktack Man*. Sifa moja ya kipindi cha Mwamko Mpya ni kwamba mtindo pamoja na ujarabati wa kifasihi ulisisitizwa. Sayansi bunilizi ilisisitizwa kuwa fasihi halisi na yenye ubunifu. Harlan Ellison aliandika mkusanyiko kwa jina *Dangerous Visions* uliochapishwa mwishoni mwa miaka ya 1960, kitabu alichokiona kama kielelezo cha mabadiliko makubwa. Toleo la kwanza lilishinda tuzo katika *The World Science Fiction Convection*. Kitabu hiki kilitokea kuwa bora na chenye utata mkubwa katika mwaka wa 1967. Mnamo mwaka wa 1970 Philip Jose Farmer aliandika riwaya yenye uvumbuzi wa hali ya juu kuhusu wakati ujao. Riwaya hii ilijulikana kama *The River world*.

Mwandishi mwingine wa Mwamko Mpya alikuwa J.G. Ballard aliyeandika riwaya kama *The Drowned World, The Burning World* na *Crystal World*. Micheal Moorcock aliandika *Behold The Man*. Miaka ya 1970 ilipelekea sayansi bunilizi kuwa ya saikolojia ya kijamii. Filamu za sayansi bunilizi ziliendelea kuwa maarufu na kuvutia watu wengi. Katika mwongo huu kazi kama vile *A Clock Work Orange, Star Wars* na *Close Encounter of the Third Kind* zilitolewa. Kupitia sayansi bunilizi pamoja na ujarabati wa kisayansi jarida la *Omni* lilichapishwa katika miaka ya 1970.

Kipindi cha Wanawake katika Sayansi Bunilizi

Kuanzia miaka ya 1970 na kuendelea katika miongo michache baadaye kulishuhudiwa mabadiliko ya kitamaduni kuhusu makundi ya kutetea haki za wanawake. Wanawake wakawa na sauti na uwezo katika utamaduni wa Kimagharibi na vilevile wanawake wakawa na nafasi katika kipera cha sayansi bunilizi mnamo miaka ya 1970 na 1980. Vuguvugu hili liliongozwa na Ursula Leguin ambaye aliibuka kuwa mwandishi wa sayansi bunilizi aliyeheshimika sana katika kipindi

chake. Mnamo mwaka wa 1969 Leguin alishinda tuzo la Hugo na Nebula kwa kuwa mwandishi bora wa mwaka wa sayansi bunilizi. Riwaya yake ikiitwa *The Left Hand of Darkness*.

Wanawake wamepiga hatua katika uandishi wa sayansi bunilizi kutoka miaka ya 1970. Kwa jumla waandishi wa kike wamechangia katika uandishi wa sayansi bunilizi katika mitazamo ya kijamii, kibinadamu na kisaikolojia katika maendeleo ya sayansi bunilizi ya kisasa. Sauti zao na mielekeo imeleta usawa na kukuza fikira ya wakati ujao katika kipera cha sayansi bunilizi. Mnamo mwaka wa 1980 sayansi bunilizi ilitawala ulimwengu katika tamaduni za kimagharibi.

Kipindi cha kukomaa kwa Filamu za Sayansi bunilizi

Filamu za *StarWars* zilienea katika jamii na kwa mitandao yote ya jamii za Kimagharibi hasa kule Uropa na Japan. Filamu maarufu za sayansi bunilizi zilikuwa *E.T Extra Terrestrial*, *Mad Max 2*, *The Thing*, *Alien and Aliens*, *Back to the Future*, *The Terminator* *Dune* na *Blade Runner*. Kipindi hicho kingine kilianzishwa katika runinga na filamu katika vyumba vya sanaa; hili lilipelekea sayansi bunilizi kuenea na kukolea katika vyombo vya habari. Kwa jumla miaka ya 1980 ilikuwa kipindi cha kukomaa kwa filamu za sayansi bunilizi. Katika kipindi hiki Filamu za *Star Wars* na *Extra Terrestrial* ziliuzwa kwa wingi sana.

Kuenea kwa sayansi bunilizi katika miaka ya 1980 kulitokana na athari za filamu ya *Star Wars*. Ambapo kulikuwa na wahusika wa kiajabu, mandhari na teknolojia hasa roketi za angani. Maendeleo haya pia yalichangiwa na tarakilishi iliyotumika mwishoni mwa miaka ya 1970 na miaka ya 1980 kutolea filamu za sayansi bunilizi. Matumizi mengi ya tarakilishi na maendeleo ya teknolojia na mawasiliano yaligusiwa sana kama maudhui ya sayansi bunilizi ya miaka ya 1980.

Wanasayansi wa tarakilishi akiwemo Ray kurzweil Hans Moravec na Vernor Vinge ambaye pia ni mwandishi wa kibunilizi walitabiri kuwa hivi karibuni tarakilishi zitazidi maarifa ya binadamu. Hata hivyo Clute (1995) anadai kwamba sayansi bunilizi hainui kupindua binadamu au jamii. Frederick Pohl alikuwa mwandishi maarufu wa sayansi bunilizi wa miaka ya 1970 na 1980 mwaka wa 1976 Pohl alichapisha riwaya kwa jina Man Plus na ikashinda tuzo ya Nebula.

Cyberpunk ambacho ni kijipera cha sayansi bunilizi kilianzishwa na mwandishi William Albson kwa kuandika riwaya *Neuromancer* ambayo ilishinda tuzo la Hugo-Nebula. Cyberpunk ni mkusanyiko changamano wa mawazo mengi ya kijamii na kiteknolojia kuhusu tarakilishi na utamaduni unaotokana na matumizi ya tarakilishi. Baada ya riwaya *Neuromancer*, cyberpunk iliibuka kuwa vuguvugu maarufu la utamaduni. Majarida kama vile *Wired* na *Mondo* pamoja na *Dark Gothic* yote yanaangazia athari za cyberpunk.

Cyberpunk iliibuka kuwa kipera bainifu cha sayansi bunilizi katika miaka ya 1980 na baadaye iliathiri sayansi bunilizi katika filamu. Athari za cyberpunk katika sinema zinadhihirika kwa kurejelea mkondo wa filamu za sayansi bunilizi za miaka ya 1990s. Clute (1995) anarejelea

sayansi bunilizi ya miaka ya 1990s kama, *Facing a New Century* katika miaka ya 1990s filamu zilishoheni wahusika majagina wenye uwezo mkubwa. Filamu hizi vilevile zilionyesha uharibifu mkubwa. Filamu hizi za sayansi bunilizi ni pamoja na *Terminator 2*, *Total Recall*, *Predator* i na ii, *Demolition man*, *Judge Dredd* na *Fifth Element*.

Miaka ya 1990 kuliibuka *Alien Resurrection*, *Independence Day*, *Event Horizon*, *Dark City*, na *Blade*. Kazi hizi zote za kibunilizi zilitabiri michafuko mikubwa. Katika miongo ya hivi karibuni riwaya za kibunilizi zenye mawazo ya kisayansi na sayansi bunilizi changamano ziliandikwa. Riwaya hizi zilihusu teknolojia, jamii za baadaye na ustaarabu. Kazi hizi pia zilishoheni maudhui ya kifilosofia, haki za kibinadamu, dini na pia wahusika wenye uasilia wa wakati ujao. Kwa kuwa maudhui haya yanapatikana katika riwaya hizi teule basi sayansi bunilizi ilipenya na kusambaa katika riwaya za Kiswahili zilizoandikwa katika Afrika Mashariki na waandishi kama K.W. Wamitila na S.A. Mohamed.

Mwandishi maarufu wa kipindi hiki ni Neal Stephenson ambaye aliandika riwaya *Snow Crash* (1992) ambayo mandhari yake ni mji wa Los Angeles. Riwaya hii ni mojawapo wa kazi maarufu za kibunilizi zinazorejelewa mara kwa mara katika miongo miwili iliyopita. Grey Bear pia ni mwandishi wa kisasa wa sayansi bunilizi, Grey ameandika riwaya ya kibayoteknolojia kwa jina *Blood Music* mnamo mwaka wa 1985 pamoja na *Moving Mars* (1993) riwaya iliyoshinda tuzo ya Nebula. Vilevile aliandika riwaya *Darwin's Radio* (1999). Bear aliandika riwaya nyingine mnamo 2003 kwa jina *Darwins Children*.

Riwaya hizi zinaonyesha tabia ya binadamu kutokana na aina mpya ya viumbe. Bear aliandika riwaya nyingine kwa jina *Queen of Angels* (1990) ambayo mandhari yake ni mji wa Los Angeles mnamo mwaka wa 2047. Dan Simmons ni mwandishi mwingine wa sayansi bunilizi ya kisasa. Dan aliandika riwaya nne za kiepiki *Hyperion* (1989) *The fall of Hyperion* (1990) *Endymion* (1995) na *The rise of Endymion* (1997) riwaya hizi zina mandhari yake katika karne ya 28 na 31. Simmons aliandika kitabu kingine kwa jina *Illum* (2003).

Vinge Vernor (1992) ni mwandishi wa kibunilizi wa kisasa aliyeandika riwaya *A Fire Upon the Deep* (1992) ni riwaya iliyoshinda tuzo ya Hugo. Mnamo mwaka wa 1999 Viuge aliandika kitabu kingine kwa jina *A fire upon the Deep. A Deepness in The Sky* (1999). Kim Stanley Robinson aliandika *Mars Trilogy Blue Mars* (1991) *Green Mars* (1994) na *Blue Mars* (1996). Riwaya ambazo zilishinda tuzo ya Hugo kwa kuwa riwaya bora zaidi za mwaka.

Vacuum Diagrams (1997) ni kazi yake Stephen Baxter ambaye ni mwandishi wa sayansi bunilizi ya kisasa. Kazi hii ya *Vacuum Diagrams* ilishinda tuzo ya Philip K. Dick kwa kuibuka riwaya bora zaidi ya sayansi bunilizi ya mwaka wa 2000. Baxter aliandika na kufaulu katika kudhihirisha mawazo ya sayansi na teknolojia katika kazi yake *Manifold Space* (2001) na *Manifold Origin* (2002). Na vile vile kazi yake S.A. Mohamed ya *Babu Alipofufuka* (2001) na kazi yake K.W. Wamitila *Bina-Adamu* (2002) kwa hivyo sayansi bunilizi ilipiga hatua si

Magharibi tu bali pia Afrika hasa Afrika Mashariki kama kipera cha riwaya katika fasihi ya Kiswahili.

Kipindi cha Milenia Mpya cha Sayansi Bunilizi

Katika milenia mpya sayansi bunilizi inaendelea kukua na kuwa maarufu pamoja na kuwa na athari kubwa ulimwenguni kote. Sayansi bunilizi ni mtandao mpana ulimwenguni kote. Makongamano hufanyika kila mwaka kusherehekea waandishi, wasanii, vitabu vipya na hadithi za awali. Mashabiki hujitambulisha na sayansi bunilizi kwa mitindo mbalimbali. Makavazi ya sayansi bunilizi na jumba maarufu limejengwa Seattle mjini Washington Marekani.

Sayansi bunilizi ina athari kubwa sana katika utamaduni na hivyo ni utamaduni wa kivyake. Sayansi bunilizi hujikita katika kushughulikia nyanja zifuatazo: jamii za binadamu, miji, tamaduni za baadaye, uvumbuzi wa kisayansi na kiteknolojia, maendeleo ya binadamu ya kiakili, ustawi wa kimaisha, roboti-tarakilishi, safari za wakati, filozofia, dini, maadili, wanawake, wanaume na mapenzi ya baadaye, uhalisia wa kisasa, vita vya baadaye, mwisho wa dunia na asili ya vitu.

Ni wazi sayansi bunilizi kutokana na usomi uliofanywa imeendelea zaidi katika mataifa ya Kimagharibi na Afrika ingawa kazi nyingi za Kibunilizi ni za wastani baadhi ya watunzi wa karne ya ishirini walifaulu katika utunzi wa baadhi ya kazi zao za Kibunilizi. Miongoni mwa watunzi waliofaulu ni pamoja na Ray Bradbury na Arthur C. Clarke, Clarke Ashton Smith, H.P. Love Craft, Henry Kuttner, Theodore Sturgeon miongoni mwa wengine. Sayansi bunilizi imeingia katika bara la Afrika kupitia waandishi kama Shaaban Robert, Katama G. Mkangi na K.W. Wamitila na S. A Mohamed. Sayansi bunilizi ya Kiswahili haijapitia katika mikondo mingi kwa hivyo ujuzi wa mtafiti kuhusu sayansi bunilizi ya Kimagharibi umetusaidia kufahamu sayansi bunilizi ya Kiswahili katika riwaya teule za *Bina Adamu* (2002) na *Babu Alipofufuka* (2001).

SURA YA TATU

Maelezo mafupi ya Uandishi wa K. W. Wamitila

Kyalo Wadi Wamitila alizaliwa mjini Machakos, nchini Kenya, mwaka wa 1966 na anaishi Nairobi anakofanya kazi katika Chuo Kikuu cha Nairobi. Masomo yake ya awali yalikuwa huko Machakos halafu akaenda Arusha nchini Tanzania. Alisomea shahada ya sanaa na uzamili katika Chuo Kikuu cha Nairobi. Baadaye, Wamitila alisomea shahada ya uzamifu katika Chuo Kikuu cha Bayreuth, nchini Ujerumani. Wamitila ni mwandishi wa tamthilia, hadithi fupi, riwaya na mashairi. Pia ni mhakiki wa fasihi ambaye amechapisha makala mbalimbali katika majarida ya kiusomi Afrika, Ulaya na Marekani.

Mwandishi ana shahada ya uzamifu katika somo la fashi. Vitabu vyake vingine ni *Wingu la Kupita* (Tamthilia 1999), *Nguvu ya Sala* (Riwaya 1999), *Kamusi ya Methali*, *Kamusi ya Misemo*

na *Nahau na Uhakiki wa Fasihi*. Bina-Adamu (2002), Pango (2003) na Musaleo (2004). K.W. Wamitila ni mwandishi wa tamthilia, hadith fupi riwaya na mashairi, pia ni mhakiki wa fasihi ambaye amechapisha makala mbalimbali katika majarida mbalimbali ya kitaaluma barani Afrika. Ulaya, Asia na Marekani.

Baadhi ya riwaya zake alizoandika ni pamoja na *Nguvu ya Sala* (1999), *Pango*, *Bina-Adamu!* (2002) *Musaleo* (2004), *Wana wa Bundi* (2005) na *Mchezo wa Mende* (2006). Baadhi ya tamthilia alizochapisha ni *Wingu la Kupita* (1999) *Pango* (2003) na *Sumu ya Bafe* (2006). Pia amehariri mkusanyiko wa hadithi fupi *Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingine* (2005) na *tamthilia ya Maisha* (2006). Kazi zake nyingine ni pamoja na *Uhakiki wa Fasihi Misingi na Vipengele Vyake* (2002) *Kamusi ya Methali* (2002), *Kamusi ya Misemo na Nahau* (2002) na *kamusi ya tashbihi, Vitendawili Milio na Mishangao* (2003).

K.W. Wamitila anaongozwa na imani kuwa nchi za kimagharibi nchi za kiafrika na ulimwengu wa tatu zinaendelea kunufaisha nchi za kimagharibi kama vile masuala ya utandawazi, hayakuletwa kuwanufaisha waafrika bali kutajirisha nchi za kimagharibi, Riwaya zake *Msimu wa Vipepeo* (2006) na pia *Bina –Adamu* zinaonyesha wazi jinsi waafrika wanavyoathiriwa na dhana kama hizi. Kufikia sasa kazi nyingine mpya ambazo ameandika ni pamoja na, *Tikiti maji* (2013) *Harufu Ya Mapera* (2012) *Mikakati ya Uhalisiajabu katika riwaya ya Kiswahili* katika makala ya Mulika (2012) na *Tikiti Maji* (2013)

Muhtasari wa Riwaya ya Bina-Adamu

Sura ya kwanza *Bina-adamu* anasimulia kuhusu kijiji chao. Anasema kwamba alipozaliwa aliwakuta watu wakikiogopa kiini cha kijiji chao hadi leo. (Wamitila 2002:7) kulikuwa na wakazi watatu tu. Mmoja ni mhubiri aliyetorokwa na mkewe kwa sababu ya ukosefu wa chakula. Mkazi wa pili ni kichaa aliyeishi kwenye kibanda. Wanakijiji wanasema kwamba kichaa huyu alikuwa mganga kabla ya wao kumfanya au kumtia kichaa. Mkazi wa tatu alikuwa hajulikani kwa jina na watu wengi kijijini. Hata hivyo, alikuwa na watoto watatu huntha walioondoka zamani na hajulikani walikohamia; kichaa aliishi kuwatafuta. Wanakijiji wanaamini kwamba wakipatikana wataleta matumaini kwa kijiji kizima. Huntha hawa walilaaniwa. Ili kuondoa laana hii sharti hawa waja laana waondolewe ulimwenguni ili kuiondoa laana kijijini. Hivi ndivyo Bina-Adamu walivyosimuliwa utotoni. Mageuzi haya yakifanyika Bina-Adamu ataishi alivyotakiwa (Wamitila 2008:8).

Bina-Adamu anaanza safari yake kwa kupuuza imani ya hapo kijijini kwamba angepatwa na madhara akikaribia kiini chao. Jagina aliamini nyanyake alidanganya sana. Mwanamume atakayeenda huko anaweza kushtukia amebadilisha jinsi na kuwa mwanamke kwa kuwa ni lazima alizunguke jabali kubwa lililoko hapo (Wamitila 2002:9) Anaanza safari yake bila kukadiria ukubwa wa jukumu lake mara tu anapotambua ukubwa wake. Sehemu hii inaendelea hadi sura ya ishirini na tatu. Hii ni sehemu ndefu sana kwa sababu inahusisha safari nzima ya Bina-Adamu msafiri. Msafiri anao wasaidizi katika safari yake.

Mmoja ni msaidizi asiyeonekana ambaye daima humuongoza kwa kumpiga makofi na mateke. Mwingine ni mwanamke anayejulikana kama Hanna ambaye anamkumbusha msafiri bibi yake kwa sababu anafanana naye sura. Bina-Adamu anapigwa teke na kuambiwa aanze safari yake ya uvumbuzi.

Anafuata viunzi vinavyokuwa vikitoa mwangaza kwa sababu kuna giza jingi mno ndani ya pango wanamoingilia. Katika kibao alichokiona kilikuwa kimeandikwa “Njia ya uhalisi) Anapoendelea anainusa harufu ya beberu na kusita kidogo. Mara analiona jitu nene lililokuwa limeandikwa UMEMO-JAPA. Alilifuata ghafla na kufuatwa na kicheko kikubwa Wamitila (2002:14).

Mara wanatumbukia kwenye mto uliokuwa na maji mengi ajabu. Ajabu ni kwamba mkondo wa maji uliwavuta wakawa wanarudi nyumanyuma tena kwa kasi ya ajabu. Mahali anapojikuta ni nchi ya Zakongwe. Huko anabadilika na kuwa mtoto mdogo, anahimizwa na babu ajiunge na watoto wenzake kucheza michezo kama vile mwajificho, kufunga ng’ombe, kufukuza wanyama wadogo msituni na kusikiliza hadithi za babu jioni.

Msafiri anafurahia maisha haya kwa sababu huko ni jana ambapo maisha ni ya raha na upendo. Hata hivyo ni lazima aendelee na safari ili kukamilisha jukumu lililo mbele yake. Kabla ya kuondoka, babu anampa mfuko ambao anamwambia autunze sana kwa sababu ndani yake mna utu, mapenzi na kiini cha kuwako kweke. Kwa bahati mbaya anachukuliwa kimiujiza na kutoka huko na kuuacha mkoba. Tukio hili linatokea siku moja wanapokuwa wakicheza mwajificho na watoto wenzake karibu na mto, analiona joka kubwa na anapokuwa akitoroka anaanguka majini na mawimbi yanambeba. Binadamu anajikuta kwenye mto wa ajabu. Hajui kuogelea lakini anajipata akielea majini. Safari hii inakatizwa na kisiki kikubwa kilichokingama mtoni. Kisiki hiki kinamgonga na ghafla kinamvingirisha juu juu kama mpira na anaanguka nchi kavu. Hapo ndipo anapokutana na msaidizi wake Hanna kwa mara ya kwanza. Wanapokuwa wakitembea wanatokezea mahali ambapo kuna majengo ambayo hayajakamilika. Kwa kuwa wanaume wote wenye nguvu wamesombwa na kuchukuliwa na Umero-Japa (uk.28) jambo hili linaonyesha madhara yaliyotokana na muungano kati ya Uropa, Marekani na Japani, Msafiri anakumbuka jitu alilokuwa ameliona huko mbeleni lenye maandishi Umero-Japa (Berfoniani 2004:3).

Kituo kingine wanachokwenda kina machimbo ya madini, bila mmea hata mmoja bali bundi wengi katika mapango. Anajulishwa kwamba hayo machimbo yalikuwa na dhahabu fedha na ulanga. Watu walihimizwa kuchimba kwa ahadi ya kulipwa lakini hawakupata kitu. Waliofaidi ni waliopora madini yenyewe (uk.29).

Msafiri anaendelea kupitia mahali mbalimbali kusikotajwa kwa jina ila kunatambulika. Katika riwaya hii bundi anaashiria mambo yanayopingana. Katika mapokeo ya Kimagharibi anaashiria hekima na werevu. Bina-Adamu anapomwona mwanamke mmoja akiwa na huyo bundi anauliza kwa nini amembeba na anaambiwa kwamba kule Ropa bundi ni ishara ya busara. (Wamitila 2001:33) ikiwa huyo bundi hawezi kufasirika kwa njia moja, ikiwa ndege huyu huashiria bahati

nzuri au mbaya, jambo hili basi humsaidia mhusika kutumia uamuzi wake kuhusu jambo zuri au baya.

Nchini Ujerumani anawapata watu walioshika tama. Nyuma yao pana jengo kubwa ambalo halijakamilika na ambalo hawataki kuliangalia. Jengo hili liliharibiwa wakati wa vita vya pili vya ulimwengu (vita vya Fyura au Hitler). Watu hawataki kulitazama jengo hilo kwa sababu linawakumbusha jana (ambayo hawataki kuikumbuka). Aidha, hawataki kulibomoa kwa sababu hawataki kufuta jana yao (Uk.36). Huko huko Ujerumani msafiri anashuhudia visa vya ubaguzi wa rangi. Msafiri anajiambia kwamba ubaguzi wa rangi huenezwa na utandaridhi. Aidha, anakumbana na Joseph Mengele na madaktari wenzake ila yeye Mengele ni maarufu zaidi. Kazi yake ni kuchunguza watu wasio na mbegu zifaazo za uzazi kisha kupendekeza njia za kuwaangamiza. Angeweza kuitwa daktari wa kifo; hufanya hivi ili kuendeleza kizazi chenye sifa nzuri. Jambo hili linatukumbusha jamii kamilifu aliyotaka kuanzisha na kuiimarisha Hitler wakati wa utawala wake. Aidha, tunakumbushwa nia ya Hitler ya kuwaangamiza wayahudi wote kutoka ulimwenguni alipokuwa dikteta.

Hatimaye kusudi la kuwafanya wanadamu wote watawaliwe kwa mfumo mmoja (wa ulimwengu) wa kiuchumi na jamii unawasilishwa katika dhana hii ulimwengu unalazimishwa kuwa kijiji. Msafiri anagundua kwamba, huko Uropa, makanisa yamegeuzwa kuwa hoteli, huku kunaonekana foleni ndefu za vijana wanaongojea kutazama sinema za kimarekani; kama vile “Star Wars, Rocky na Missing in Action”. Msafiri anaambiwa kwamba hawazitazami, sinema za kwao kwa kuwa waafrika wamekengeuka. Hawajiamini na hawaoni kuwa kitu chao ni kizuri. Jambo hili tunalionga sio kwa sinema tu bali hata vile wengine hupendelea mitindo ya nguo za kigeni, na hata kuongea.

Si ajabu basi waafrika wanaogopa kuchukua nafasi yao katika kijiji (ulimwengu) na kutosheka kukaa pembeni. Ni wazi kwamba waafrika wana jukumu kubwa katika kuamua watakaa wapi pembeni au kwenye kiini. Nchini Urusi ingawa watu ni maskini wenye bidii na mkono wazi msafiri anashuhudia utu na matumaini. Msafiri anapewa mfuko uliojaa vitabu kama zawadi. Kimojawapo cha kitabu anachopewa kinahusu hadithi ya mzalendo anayejulikana kama Che. Ni hadithi ya ukombozi na ufahamu. Che ni jasiri anayesimama wima kupambana na Yanguis nguvu kuu katika ulimwengu (uk.81).

Baadaye tunamwona Bina-Adamu akiwapatia kitabu hiki watu katika mojawapo ya nchi anazozizuru ambao anaona kwamba wanahitaji ukombozi na viongozi kama Che. Urusi ni tofauti na kwingine ambako watu wanacheka kipindi cha ukimya kwa sababu kila mtu atakuwa anategemea teknolojia ya mashine na kwa hivyo hatakuwa na haja na binadamu mwenzake.

Msafiri anazuru Japani kwenye ishara ya maafa yaliyowapata watu wengi, wamelemaa mikono na miguu. Watoto wengi anawaona wana alama kama waliomwagiwa kitu fulani kilichowachubua ngozi, (Wamitila 2002, 46). Inasemekana kwamba P.P (Marekani) alitupa bomu fulani na watu wengi wakafa na wengine kuathirika vibaya sana. Tangu wakati huo watoto

wanaozaliwa ni vilema. Kuna magari mengi ambayo hayatumiki tena lakini ambayo anaambiwa yana soko kubwa upande wa chini kwa sababu huko ndiko wanapotupa vile vitu ambavyo hawahitaji tena. Karibuni samaki wabichi watakuwa wakiuzwa huko kwa sababu ingawa kuna maziwa mengi ya kuvua, wale wanaouziwa (waafrika) hawana idhini ya kuvua kwenye “international waters”. Msafiri anashangaa kama hiyo ndiyo maana ya “free market economy na liberisation”. Anashangaa kama hayo ndiyo maendeleo na kama ndio maana ya ulimwengu kuwa kijiji.

Msafiri anapotembea kutoka Bara moja hadi lingine anakumbana na watu ambao wamekuwa maskini kwa sababu ya uchumi unaoitwa wa soko huru. Wanamwita Bina-Adamu mkombozi wao na kumtuma kwa P.P; wengine wanamwambia amwambie P.P akimwona kwamba hawajasahau mabaya yote aliyowatendea. Jagina anatembelea kijiji chao ambacho kinawakilisha Bara la Afrika. Anapumzika huku kwa muda mrefu katika kijiji (bara la Afrika). Kuna nyumba (nchi) zifikazo hamsini na mbili, nyumba nyingi zimeinamiwa na miti mbalimbali ya matunda kama vile miembe, mipapai, michungwa na mingine mingi. Kila kiongozi anakaa juu paani anakochana matunda kwa urahisi na kuwatupia watu walioko chini ambao ndio waliomshikia ngazi ya kupanda juu. La kusikitisha ni tabia ya wengi wa viongozi wa nchi hizi.

Baada ya kula na kushiba, wao huyatupa makaka, makokwa na maganda huku chini yanakong’ang’aniwa na umati mkubwa ulioko chini. Baadhi yao hata huiba matunda na kuyahamishia kwingine labda ughaibuni. (Wamitila 2002:67-68).

Hawa viongozi wa kiafrika wanao uvimbe kwenye nyuso zao. Uvumi unasema kwamba walipigwa kwa jiwe lililotupwa na Goliath! Ajabu ni kwamba kisa cha Bibilia husema kwamba Daudi ndiye aliyempiga Goliath (Wamitila (2002:70-71) P.P kama anavyowahangaisha watu kwingineko ndiye aliyehusika na uvimbe huo. Wengi wa waafrika ni wanyanyaswaji. Nyumba za kijiji hiki zinafanana lakini wakazi wake hawashirikiani ili kujitatu. Wanasema kuwa kila nyumba ina kiongozi wake na hawataki kuingilia kati (Wamitila 2002:72).

Hapa msafiri anairejelea mikataba mibaya kati ya nchi mbalimbali za Bara la Afrika licha ya kwamba nchi za Ulaya zinaendelea kuungana. Waafrika nao wanaendelea kutengana kwa sababu za kibinafsi, ufisadi na ulafi wa viongozi. (Wamitila 2002:73).

Nyumba (nchi nyingine) ambayo jagina anaitembelea ina maajabu yake. Kiongozi wa hii nyumba ambaye ni dikteta anaiogopa historia. Nchini humu, jagina anayaona magofu. Anapouliza hayo magofu ni ya nini anaelezwa na mzee mmoja kwamba ni ya kituo cha usomi kilichofungwa. Hii ni kwa sababu hawakutaka kiendeleo na utafiti wake wa kuifunua historia kwa kila mtu walisema malengo yake ni mabaya.

Baadaye hospitali inaanzishwa lakini pia inafungwa baada ya dawa kuuzwa na wanasiasa ili wapate pesa za kufanyia biashara! Wanapoulizwa kwa nini kufanya vile wanasema kwamba sio

neni. Eti hayo ni matatizo ya kawaida yanampata kila mtu katika dunia nzima wanayoita kijiji, “global village” (Wamitila 2002:87).

Mzee huyu anaendelea kumjulisha jagina kwamba nyakati zinazoendelea siku hizi katika hali yake ya sasa ni maangamizo. Hamna cha “global village” tena bali ni uharibifu wa sayari yenyewe pamoja na wakazi wake. Kulingana na huyo mzee hiyo ni “global pillage” (yaani uporaji wa ulimwengu). Mzee huyu pia analalamika kuhusu shirika la (IMF). Anasema kwamba jamii zimekosa uhuru wa kuamua hatima yao kwa sababu uwezo huo umeingiliwa na mtaji unaoweza kuingia na IMF haliwezi kujipangia mambo yao kwa sababu hawajui ni lini watapata pesa (Wamitila 2002:87).

Jagina anapokuwa anatembea karibu na ukingo wa bahari anakutana na watu wanaolalamika kwamba mafuta yamemwagwa baharini na kuwaua samaki wote. Kwa kufanya hivi, wale waliomwaga mafuta watapata sababu ya kuuza samaki wao wa makopo. Hawa hawa ndio wanaotupa nyuklia huko juu.

Jagina anapouliza kwa nini watu hawashirikiani na kupinga vitendo kama hivi anaambiwa kwamba tatizo ni ubinafsi na ukabila. Kila mtu na ndugu zao wanakwea juu ya mti wa matunda na kuanza kula matunda na wenzake wachache. Ndugu zake wanajua kwamba huyu ndugu yao anaiba hata mbegu. Wangekuwa na mbegu, wangepanda na kuiongezea idadi ya mimea na angaa kuhakikisha kwamba keshowe matunda yamewafikia watu wengi zaidi (Wamitila 2002: 91).

Ubaya ni kwamba kiongozi huyu amejiumba na waimbaji ambao hutunga tenzi mpya na kuzikariri kama sala ya bwana eti kwa sababu yeye hupenda kusifiwa. Huyu kiongozi anajulikana kama Musa wa leo na watu wakiwemo watoto wa shule wamefunzwa hivyo. Inasemekana kwamba yeye ni kila kitu na akiondoka ataliliwa sana. Huyu kiongozi anafananiwa na Musa wa Biblia aliyewaongoza na kuwatoa wanaisraeli utumwani Misiri. Baadaye usiku Jagina aanza safari yake tena baada ya kupumzika kwa muda mrefu. Babu yake wa Zakongwe anamletea mkoba wake mlimokuwa na utu.

Anapopita karibu na ziwa fulani anashuhudia watalii ambao wamezivua nguo zao huku wakicheza na wasichana wadogo sana wa kiafrika waliovaa visketi vinavyofika magotini na viblauzi vinavyoning'inia tumboni, aidha kuna wazungu wengine wanaonasa matukio hayo kwa kamera zao za video (Wamitila 2002:108). Mkondo wa mwisho wa safari ya Jagina unaanza; anafahamishwa kwamba akitofanikiwa kuwapata wale huntha na kurudi nao pale kijijini basi hakuna matumaini ya kijiji chao. Ikiwa hatawapata anaambiwa ahakikishe amewajua. Hii ni kwa sababu hawa wasichana-wavulana si dhahiri bali ni vielelezo vya matatizo makuu yanayokumba nchi za Afrika.

Ndio maana anaambiwa kuwa hata kama hataweza kuwashika kwa sababu mwandishi anajua si dhahiri au halisi, hayashikiki wala kubebeka ahakikishe kwamba ameyajua matatizo hayo. Hii ni

kwa sababu amezuru kwingi na kuona mengi sasa anaweza kufikia hitimisho au uamuzi fulani kuhusu shida hizo (Wamitila 2002:110).

Jambo hili linadhihirika zaidi wakati Jagina anaambiwa kwamba ni muhimu waukabili uhalisia wao na kujaribu kubadilisha hali zao badala ya kukimbilia ng'ambo kwa sababu wasipopata suluhu kwa matatizo ya nchi yao watakimbia milele kama vile jagina anavyofanya. Katika safari hii anapitia karibu na bahari na akawaona watu wakivua samaki kwenye 'international waters' ili wawauze wakiwa kwenye mikebe. Aidha, analiona jahazi lililo na maandishi AMISTAP I. anakumbuka kwamba hili ni jina la meli iliyotumiwa ili kuwabebea watumwa kuwapeleka nchi walikokwenda kuhudumu katika mashamba ya mamwinyi zama za utumwa. (Wamitila 2002:116). Historia inaletwa mbele ya macho yake kwa muhtasari. Bahari tena ingawa si ya kweli bali ya ishara kama vile Hanna amwambiavyo ili kutoka nchi ya Jana (Afrika) na kwenda nchi ya leo (Marekani). Anapofika Edeni ya pili (Marekani) anawaona wanaume na wanawake wanaokaa wakiwa uchi. Anapowauliza kwa nini wako hivyo wanamwambia kwamba wanakaa hivyo ili kuhisi kama wako 'Jana' kwa sababu leo yao haina furaha. Kwa kukaa uchi wanatafuta furaha kwa kujikumbusha maisha ya kitamaduni ya kiafrika. Ili kusisitiza jambo hili, mwandishi anatusawiria baadhi yao wakiwa wanakaa juu ya mti kama wanyama. Wanahisi wako pweke na hawana mahusiano ya kibinadamu kwa sababu wametupa mkoba wao kama ule jagina alipewa Zakongwe na babu. Hawana utu au ubinadamu wowote, hata jagina anaogopa kwamba watauona mkoba wake na kudai ni wao.

Msafiri anapotembea katika kijiji cha wakaazi waafrika, anawakuta watoto wakicheza kandanda makaburini na hakuna aneyejali kuwakanya. Hii ni kwa sababu wenyeji wanataka wageni waone na kupigia swali jambo hilo kwa sababu watu wa nje hawajui kwa nini kuna makaburi mengi hapo. Watu waliozikwa hapo ni watu weusi waliokufa baada ya kutumiwa kama panya wa maabara katika majaribio ya dawa fulani. Watafiti hawa wa kimarekani hawakufanya majaribio na watu wa jamii yao bali na waafrika. Jambo hili linaonyesha jinsi waafrika wametumiwa na wanavyotumiwa hata leo na wamagharibi ili kutimiza malengo yao kwa manufaa yao tu. Jagina anaambiwa kwamba watu hawa wanaishi katika urazini wa kuwili na wao hujifua kupitia machuo ya wengine na pia kuishi pembeni kwa bahati mbaya hiyo ndiyo tanzia ya rangi kinyume na wamarekani wazungu wanaoishi sana. Wamarekani weusi wanaishi leo. Hawaishi katika ndoto bali kwa ulimwengu wa kweli kwa uhalisia. Msafiri anaporudi mjini anaingia katika kiwanda kimoja cha utafiti. Mwana sayansi mmoja anamwelezea kwamba wanaishi kesho na mtondo. Hawaishi kwa matumaini bali kwenye uhalisia wa kisayansi huku wamesahau jana kabisa. Kwa mujibu wa maelezo ya mwanasayansi huyo, ulimwengu unaweza tu kuokolewa na shujaa ambaye anajitegemea na kuishi kivyake. Binadamu huyu atakuwa amejikomboa na migororo ya historia na 'uchafu wa utamaduni'.

Huyu ni binadamu aliye na ujasiri wa kuasi jana. Hata hivyo sauti iliyomo katika akili ya binadamu inakataa kauli hii na kumwambia kwamba jamii inayoisahau historia yake inashindwa kujieleza. Hiyo ni jamii ghibu, ambayo haipo na inayotajika kwa jina tu. (Wamitila 2002:129).

Hatimaye msafiri anatokea mahali kuliko kwenye uwazi analiona jamaa fulani likiwa limeketi. Na kuweka mikono yake kwa namna iliyowafanya watu wengine wajazane katika duara. Watu hawa ni wa rangi tofauti. Baada ya muda lile pande linakunja mikono yake lakini wale watu wanabakia palepale walipokuwa (Wamitila 2002:147). Butwaa isiyomithilika inampiga msafiri anapogundua kwamba lile jamaa ni toto tu. Linakula hamburger huku vipande vipande vikiwaangukia wale waliokuwa wakimwambia. Linakula kwa pupa huku likitiririkwa na nyute pande zote mbili za ndomo.

Anajulishwa kwamba huyo ndiye Yanguis anayejulikana kwa majina mengine kama ‘mjomba’ au Peter Pan, hiyo ndiyo sababu yeye hutupa mawe. Anaambiwa kwamba watoto wako sawa lakini kuna tofauti moja kuu kwa sababu watoto wote hukua ijapokuwa Peter Pan, yeye atabakia mtoto milele (Wamitila 2002:151). Baada ya muda mfupi lile toto linasimama na kumwambia msafiri kwamba linafahamu kwamba alikuwa akimtafuta P.P; anamuuliza atafanya nini kwa sababu sasa amemjua. Bina-Adamu anamwambia kuwa atawaambia wenzake wasifanye kosa la kumpa unga. P.P anamjulisha msafiri kwamba atakuwa anapoteza wakati kwa sababu tayari amewaingia akilini kabisa, walimwengu. Anapenda kuwambia kuwa anahisiwa kwingi hata asikokuweco. Kwa kweli, P.P anamwambia Jagina, kutokuweco, kwake ndiko hata kuwako kwake (Wamitila 2002:153).

Katika sura ya ishirini na tatu na ya mwisho baada ya P.P kutoweka, msafiri anasikia vicheko vya wale huntha anaowatafuta na ambao hawaoni ila kusikia sauti zao tu. Anataka kuwakimbiza lakini babu anamkataza, anamwambia kwamba ni kazi bure kuwakimbiza kwani hawapo na hutokea katika matendo na fikra tu. Huyu ni yule babu wa Zakongwe anamwambia msafiri ni bure kuwafukuza huntha wasioonekana. Anamjulisha kwamba wamekwenda kila mahali alikopita na kwingineko wamezaa watoto na kuwaacha huko.

Bina-Adamu anamuuliza babu kama anawajua majina lakini anamwambia kwamba yabidi yeye na baadhi ya wanaojulikana ni kama mwanakabila, Bin rangi, mkengeushi na wengine wengi na ni lazima waangamizwe ikiwa kijiji chao kitapata fanaka.

Babu anamjulisha Jagina kwamba jamii nzima ielimishwe upya kuanzia chini hadi juu; mtoto hadi mzee na watu wote kwa jumla. Kwa kufanya hivyo kila mtu atajua kwamba hakuna huntha waliosababisha matatizo yao bali ni jukumu lao wenyewe kujitazama na kujirekebisha pale inapohitaji. Bina-Adamu anasikia sauti nyingine ikimwarifu kwamba wanahitaji kujuana kiuchumi, kisiasa na kijamii. Pia wawe na umoja ili waweze kumfunga yeyote yule. Wakishirikiana kama vile tusomavyo katika hadithi ya Gulliver (Wamitila 2002:154-155). Wakifanya hivi wataacha kuishi pembezoni mwa kijiji, itabidi wawe nguli kupambana na hasidi wa kijiji ambaye ni “Global villain” yaani mhalifu wa kijiji dunia.

Sayansi Bunilizi katika Riwaya ya Bina-Adamu

Riwaya ya Bina-Adamu imesheheni sifa za sayansi bunilizi ambazo ni pamoja na sayansi na teknolojia, uvumbuzi safari za angani na vita vya dunia. Kama inavyodhihirika kwenye riwaya kwa kuzingatia vipengele vifuatavyo:

Mtindo: Riwaya ya Bina-Adamu imetumia mitindo mbalimbali ambayo inaafiki sayansi bunilizi kama vile ya kiepiki ambapo msimulizi anatembea katika safari ya uvumbuzi na anatembelea sehemu mbalimbali na kuvumbua matukio tofauti tofauti. Katika riwaya ya Bina-Adamu, ubunilizi wa kisayansi unajitokeza pale ambapo kuna mtindo wa matumizi ya usimulizi usioaminika, kuna usimulizi kumhusu kichaa ambaye alisemekana kuwa mganga kabla ya kubatizwa kichaa. Vile vile kuna masimulizi ya mkazi ambaye hakujulikana kwa jina na alikuwa na watoto watatu huntha waliotoweka na ndio wanasakwa na msimulizi.

Matukio ya kiajabu yamebainika katika riwaya Bina-Adamu ambapo msimulizi anatumbukia majini na badala ya kuzama anaelea juu juu, na mkondo wa maji unarudi nyuma badala ya kwenda mbele kwa kasi. Msimulizi pia anasema kuwa mwili wake ulibadilika na akawa mtoto. Kuna matumizi ya utabiri ambapo babu anasimulia kisa cha wakati ujao cha nyoka mkubwa na watu watakaobeba moto kwenye mifuko ambavyo vinarejelea reli na uvumbuzi wa kiberiti.

Utabiri mwingine unaegemea sayansi bunilizi ambapo inatabiriwa kuwa huenda maji ya mto yakakaushwa na jua na hata hali ya hewa kubadilika na maji kugeuka theluji tupu hali hii ni kupitia maendeleo ya sayansi na teknolojia. Kuna hali ambayo haibainiki iwapo msimulizi alikuwa katika ndoto au ilikuwa halisi, kuna masimulizi yasiyoaminika pale ambapo nyanya anasimulia kuwa kulikuwa na jabali ambalo yeyote ambaye angelizunguka angebadilika jinsi yake. Hii ni sifa inayoegemea sayansi bunilizi. Matukio mengine ya kiajabu ni pale ambapo mtembezi msimulizi anapigwa makofi na mateke na watu wasioonekana.

Kuna kisa kumhusu mfalme aliyekuwa uchi ilhali raia wake walimuona kavaa nguo mpaka mtoto mdogo anagundua kuwa mfalme alikuwa uchi, tukio lingine lisilo la kawaida ni pale msimulizi anaiona mikono yake ya mtu mzima ilhali vyanda vyake vilikuwa vya mtoto hali hii inaukosa uhalisia sifa ambayo inaitambulisha riwaya hii kuwa na sifa za sayansi bunilizi. Matumizi ya mbinu rejeshi ambapo msimulizi anakumbuka hadithi aliyosimuliwa na babu yake kuhusu kuzaliwa kwake akiwa amelifumba jicho la kushoto na ikamshughulisha nyanyake msimulizi mpaka jicho likafumbuka hili ni tukio la kiajabu linalotambulisha riwaya ya *Bina-Adamu* kuwa sayansi bunilizi.

Wahusika: Wahusika wanaopatikana katika riwaya ya Bina-Adamu si wa kawaida na wanadhihirisha sifa za sayansi bunilizi. Baadhi ya wahusika hawa ni pamoja na mhusika kichaa ambaye tunaambiwa alikuwa mganga kabla ya wanakijiji kumbatiza kichaa; anaaminika kuwa alikufa miaka mingi iliyopita. Aidha inasemekana kuwa kichaa huyu aliishi upande wa pili

kwenye kibanda kilichofanana na kidungu cha kuwingia ndege. Kuna mhusika ambaye aligeuka na kuwa kunguru msimulizi alipomkaribia, alidaiwa kuruka na kwenda kutua juu ya mti.

Katika riwaya ya Bina-Adamu kuna wahusika wasioonekana na wahusika sauti ambao wanasikika tu na kumpiga msimulizi makofi. Wahusika majitu ambao si wa kawaida wametumiwa katika riwaya ya *Bina-Adamu*. Kuna jitu lenye miguu mikubwa ajabu na linarefuka ghafla. Dr. Joseph Mengele ni mhusika ambaye matendo yake yanaafiki sayansi bunilizi kwani anachunguza aina za watu walio na mbegu zifaazo na zisizofaa hivyo maendeleo ya sayansi na teknolojia yanayoegemea sayansi bunilizi.

Wahusika huntha wanaegemia sayansi bunilizi kwani wamekiuka mipaka ya kimaumbile ya kuwa mwanamme au mwanamke na badala yake kupitia mabadiliko ya kijenesi. Wamesheheni sehemu zote nyeti kike na kiume kwa pamoja, jambo hili linakosa kubainisha kati ya uhalisia na utohalisia. Wahusika wasichana wavulana ni wa kiajabu na si wa kawaida kwani hawabainishi wazi sifa ambayo inaegemea sayansi bunilizi. Katika riwaya wahusika hawa hawaonekani bali ni vicheko vyao tu vinasikika.

Mwanasayansi: Huyu ni mhusika ambaye anawakilisha sayansi bunilizi kwani anashughulika na utafiti na uvumbuzi wa kisayansi ili kuleta maendeleo ya sayansi na teknolojia. Mhusika Hanna ni wa ajabu kwani anatoweka na kisha kutokea ghafla hali ambayo si ya wahusika wa kawaida. Watu waliokuwa wameketi juu ya nyumba na wote walikuwa na uvimbe kwenye vipaji vya nyuso zao na ambao ulikuwa na ukubwa uliohitilafiana. Hawa ni wahusika wasio wa kawaida na hivyo wanaegemea sayansi bunilizi.

Wakati: Nyakati zilizotumiwa katika riwaya hii ni za wakati uliopo na wakati njao; kwa mfano msimulizi anaambiwa kuwa ulimwengu utaangamia siku atakayompua mtoto. Kama ilivyo sifa ya sayansi bunilizi riwaya hii ya Bina-Adamu imetumia utabiri ambapo babu anasimulia kisa cha mwanamke mmoja mtabiri aliyetabiri kuja kwa watu watakaokuwa wametia moto mifukoni na nyoka mrefu atakayenyiririka kutoka kisiwani hadi ziwa la Sango. Kuna matumizi ya visasili vinavyosimuliwa, kwa mfano kuna kisasili cha ndege na kinyonga waliotumwa na muumba kupeleka ujumbe kuhusu maamuzi yake kwa maisha ya binadamu. Wakati usio maalum unadhihirika katika riwaya hii ambapo msimulizi anashindwa kubaini iwapo anatembea kuelekea leo au kesho. Msimulizi anadai kukaa mahali fulani lakini hakuweza kubainisha muda kamili alioweza kukaa mahali hapo.

Maudhui: Maudhui katika riwaya ya Bina-Adamu yanaegemea yale ya sayansi bunilizi ambapo kuna maudhui kama yufuatayo: Vita vya dunia-katika riwaya ya Bina-Adamu kuna ishara ya vita hivi ambapo kuna jengo lililoharibiwa kwa mizinga ambayo ilidaiwa kutupwa na watu kutoka nje hasa P.P wakati wa vita vya Fyura. Kuna filamu zinazosheheni maudhui ya vita kama vile 'Star Wars', 'Rocky V' na 'Missing in Action'. Katika filamu hizi yanayorejelewa ni vita vya angani na vita vya baadaye ambavyo vitakuwa vibaya zaidi kutokana na maendeleo ya sayansi na teknolojia yanayopelekea uvumbuzi wa zana hatari zaidi za vita. Kuna maudhui ya vita

ambapo mabomu ya atomiki yalitupwa na kuwaua watu wengi na wengine wakaathirika kwa kuwalemaza, wale wanaozaliwa baadaye haya ni matokeo ya sayansi na teknolojia na athari zake katika jamii.

Kuna maudhui ya sayansi na teknolojia ambapo vitu vingi vimevumbuliwa na binadamu pia. Kuna friji ya kuhifadhi vitu kwa muda mrefu bila kuharibika na pia kompyuta ya kutuma barua ndogo ndogo. Kuna pia daktari wa kifo anayechunguza watu walio na mbegu nzuri ili kuendeleza kizazi chenye sifa nzuri wasio na unyonge. Jamii zilizoendelea kiteknolojia na kuwa na uwezo wa kuchukua kwa kutumia idhaa kama vile CNN, BBC CFI na DW. Maudhui haya ni thibitisho la sayansi bunilizi katika riwaya hii.

Maudhui ya utafiti yamedhihirika katika riwaya watafiti wengi wako ndani ya jengo lenye mashine nyingi wakifanya utafiti ili wasiachwe nyuma na teknolojia. Mataifa yaliyoendelea yunavumbua vitu vipya na kuviuza vilivyopitwa na wakati katika mataifa yanayoendelea. Maudhui ya utafiti yamepelekea uvumbuzi wa matumizi ya mashine za roboti zilizorahisisha mambo kwani binadamu ni mzembe. Hejemonia ni maudhui mojawapo ambapo nchi zilizoendelea na kupiga hatua kiteknolojia zinatawala nchi ambazo hazijaendelea na hivyo nchi zilizoendelea zinaongoza sekta zote zikiwemo uwezo wa kifedha duniani.

SURA YA NNE

Maelezo mafupi ya Said Ahmed Mohamed

Said Ahmed Mohamed ni mwandishi aliyefanikiwa katika utunzi wa tanzu tofauti kama vile ushairi, tamthilia, riwaya na hata hadithi fupi. S. A. Mohamed alizaliwa Disemba 12 mwaka wa 1947 huko Unguja (Zanzibar). Alipata elimu ya msingi na shule ya sekondari visiwani Zanzibar kisha akapata shahada ya B. A. Education na uzamili katika Chuo Kikuu cha Dar-es-Salaam, Tanzania. Baadaye alipata shahada ya Ph.D (uzamifu) katika isimu ya Kibantu kutoka Chuo Kikuu cha Leipzig, Ujerumani. Amefundisha katika Chuo Kikuu cha Nairobi bewa la kikuyu, Chuo Kikuu Moi kabla ya kwenda Chuo cha Osaka, Japan. Alifundisha katika Chuo Kikuu cha Bayreuth, Ujerumani na kwa sasa amestaafu.

Katika nyanja ya utunzi, ametunga katika nyanja zote. Mohamed alianza kutunga mashairi na hadithi fupi, huku akiwa mwanafunzi wa shule ya msingi mnamo miaka ya 1960; alishiriki katika mashindano ya uandishi wa hadithi fupi za Kiswahili yaliyoanzishwa na idhaa ya BBC. Baadhi ya kazi zake ameandika riwaya, kama vile *Asali Chungu (1977)*, *Utengano (1980)*, *Dunia Mti Mkavu (1980)*, *Kiza Katika Nuru (1988)*, *Tata za Asumini (1990)* *Babu Alipofufuka (2001)* *Dunia Yao (2004)* na *Nyuso za Mwanamke (2010)*, *Mhanga Nafsi Yangu (2011)* na *Mkama Ndume (2013)*. Kwa upande wa tamthilia ametunga *Pungwa (1988)*, *Amezidi (1995)*, *Kitumbua Kimeingia Mchanga (2000)* *Janga La Werevu (2011)* na akishirikiana na profesa Kitula King'ei akaandika *Posa Za Bi Kisiwa (2007)*. Hatimaye alitunga tamthilia ya *Kimya, Kimya, Kimya! 2011*.

Said Ahmed Mohamed ameandika *Kunga, za Nathari ya Kiswahili (1988)* kusanyiko la hadithi fupi, *Sadiki Ukipenda (2002)* *Si Shetani si Wazimu (2005)* *Mfuko Mtupu na Hadithi Nyingine (2006)*, *Arusi ya Buldoza na Hadithi Nyingine (2006)*. Kwa ushirikiano na Ken Walibora wameandika *Kiti cha Moyoni na Hadithi Nyingine (2006)* na *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine*. Vile vile alishiriki katika uandishi wa vitabu vya shule za upili vya lugha kama *Stadi za Kiswahili (1988)*. Ameandika pia makala kadha za tahakiki kuhusiana na fasihi ambazo zimechapishwa katika majarida ya kimataifa.

S. A. Mohamed anashughulikia matatizo ya Waafrika hasa jamii za Afrika Mashariki, kupitia lugha ya Kiafrika-Kiswahili. S.A Mohamed ametumia fasihi kama silaha kupigania maslahi ya wanajamii sawa na waandishi wengine wa miaka ya themanini nchini Tanzania.

Muhtasari wa Riwaya ya Babu Alipofufuka

Riwaya ya *Babu- Alipofufuka* inahusu mhusika K, wazazi wake walifanya kazi kwa tajiri mmoja. K, ni fadhili na alijaa ubinafsi na dhalimu. Anajivunia uhusiano wake na wafanyi biashara wenzake maarufu kutoka Uingereza na India (Mohammed 2001:28-48). Hajali kwani anadai kulindwa na Proteus, kiumbe wa kiajabu anayelinda na kutawala wote wenye nguvu na mali.

Riwaya ya *Babu Alipofufuka* inianza kwa mzuka aliyefufuka akitaka kuzungumza na kilembwekweza chake kwa jina la K. Kuna pingamizi kwa sababu K. haamini kwamba wafu hufufuka. Mzuka anajaribu kumfikia K kwa kumwita na kumtolea ishara na kumpigia kelele ingawa hafui dafu. K anaye mbwa kwa jina doggy ambaye huandaliwa vyakula vinono huku binadamu wanalala njaa. Siku chache zilizopita chakula kikiwekwa kwenye sahani na mtu kuondoka kwa dakika chache sahani huwa tupu. Doggy hubaki kubweka kwa njaa huku ikifikiriwa amekila kile chakula. K. anaona kama mazingaombwe asiyoyaelewa, jambo hili linamshangaza na kumghadhabisha sana K mpaka anawafuta wafanyikazi wengi kazi kwa kudhani ndio hukiiba chakula hicho. Mzuka ameona kuwa ni wajibu wake kukichukua kile chakula na kuwapelekea watu wasio na chakula. Mwishoni mwa sura hii K anaugua ugonjwa wa tumbo na kuharisha ghafla.

Katika sura ya pili na ya tatu K anaelekea Neo- Casino ambapo anakutana na marafiki zake wa kutoka nchi za kigeni. Hawa huchukua mashamba ya wananchi, wanacheza kamari, kuuza magari yaliyokwisha kazi kwao na kushiriki safari ya kuelekea Neo- Casino. Mzuka anamtokea K kwa kuingia kwenye nafsi ya dereva wake anayejulikana kama Mzula. K haamini huyo ni babu yake lakini mzuka anajaribu kumsawishi. Hatimaye mzuka anamwambia kwamba apende asipende yeye ni babu yake na atakuwa akimtokea kila wakati atakapo hadi atakapomaliza kumzindusha.

Mambo yasiyo ya kawaida yanatokea Neo-Casino, Wanaume wote wapangiwe wasichana wa kuwafurahisha wakila chakula cha huko ambacho huliwa kwa zamu na kila mtu na kikiwa kibichi. Mradi wa ujenzi wa klabu cha kisasa kiitwacho FKK unajadiliwa na washiriki wa kundi

hili la kushangaza na kwamba wale watakaokuwa wakienda FKK watakuwa wakiingia huko wakiwa uchi- mzuka anasikia na kuona kila kitu hivyo anamuonya K kuhusu mpango huu lakini K haonyeki. Basi mzuka anapendekeza kwamba waiite hiyo klabu jina linaloafiki shughuli za huko kama vile Giningi au Uchawini.

Sura inayofuata K anaondoka Neo- Casino na kuelekea kwa mpenzi wake Zuhura Mapozi. Huyu ni aliyekuwa mkewe Sururu ingawa K alishamnyakua. Mzuka anamwandama na kumtahadharisha K kuhusu vitendo vyake na vya wenzake. Njiani K anadai kufuatwa na viwiliwili vya watu anaoamini wanamfuata ili kumdhuru. Kwa Mapozi anakaribishwa na kuandaliwa 'vinono anamwahidi Zuhura milioni sabini ili afungue duka la mlango wa mbele la kuuza peremende na vitamu vitamu vingine.

Hata hivyo, sherehe zote zinakatika ghafla wakati Zuhura Mapozi anapomwambia K kwamba ana wasiwasi juu ya mumewe Sururu baada ya kujulishwa na pepo/shetani wake Msumari kwamba Sururu anajiandaa kulipiza kisasi. K anaposikia jina Sururu ghafla- tumbo linamtibuka na anaanza kuendesha. Mzuka naye hamwachi na K anaishia kuwa na usiku mbaya.

Katika sura ya tano K analalamika kwamba tangu kukutana na babu hayaelewi maisha yake tena. Wakati unamwingia na kumtoka tu. K anafanya mazoezi ili kutunza siha yake ila mazoezi anayofanya ni tofauti na mengine. Katika ukumbi wake wa mazoezi ametengenezesha nguzo moja nene ya chuma ambayo ameweka shilingi milioni tatu. Kila siku nguzo hiyo hupakwa girisi ili iteleze na kuweka ugumu katika kuipanda; kinachomkasirisha K ni kwamba kila siku badala ya kupiga hatua kwenda juu, anateremka. Ukweli huu unamkalia vibaya sana K kwa sababu ile hamu ya kwenda juu na juu zaidi mpaka kufika kileleni ni ndoto inayokamatana na pumzi zake kama uhai wake.

Sura ya sita, ni katika ofisi ya K ya kifahari na ya kisasa. Afikapo ofisini, K. anaifungulia mashine ya video ambayo hurekodi yote yanayotendeka ofisini kabla yake kufika. Siku hii, tofauti na zingine anaona jinsi hao anaowaita mahasimu wake walipokuwa wanapigana na askari wakijaribu kuingia ofisini mwake. Mzuka naye anakuja na maagizo yake. Anamwamrisha K aanze kufungua majalada ambayo yamerundikana kwa kutoshughulikiwa. K anafanya hivyo shingo upande; majalada yamejaa malalamiko ya watu mbalimbali walionyimwa haki yao na kudhulumiwa. Kimiujiza, mzuka anamwambia yaliyo kwenye majalada hayo yote bila kuangalia. Mzuka anasema kwamba zamani pengo kati ya matajiri na maskini lilikuwepo lakini leo katika uongozi wa akina K matajiri wamekuwa wakwasi na maskini wamekuwa wachochole. Mzuka anamjulisha kuhusu jalada la pili lenye malalamiko juu ya mashamba ya watu kuchukuliwa na jinsi nyumba za watu zilivyoharibiwa na buldoza la serikali, lazima watu walipwe fidia. Hii ni kwa sababu maafisa wanaotoa vibali vya ujenzi wanapokea hongo na kuwaruhusu watu kujenga ovyo.

Mfumo wa elimu ni chanzo cha malalamiko mengine. Kuna ubaguzi kati ya shule za watoto wa matajiri na za wale maskini. Katika yale majalada kuna moja lililo na picha za binti yake K

anayejulikana kama Kidawa akiwa uchi. Inashangaza kwamba K anapoziona zile picha haoni kama kitu bali anasema kuwa bintiye akitaka kujiuza, mwili ni wake. Anasema kwamba zile picha ni ithibati kwamba klabu chao cha FKK wanachokianzisha kitafanikiwa kwa sababu kuna watu ambao tayari wameanza kupigwa picha wakiwa uchi. K anasema kwamba hajali kwamba watu wanalalamika kuhusu dhuluma mbalimbali. K anatupa taswira ya jinsi viongozi wamedidimiza jamii kwa kutojali, kutofanya kazi na kukosa uwajibikaji kazini.

Sura ya saba K anakaribia kurukwa na akili kwa sababu shilingi milioni tatu alizotundika nguzoni zimechukuliwa na mwanawe Bamkubwa. Kinachomkasirisha zaidi si pesa zilizoibwa bali ni vile yule aliyezitoa alivyoweza kupanda juu ya nguzo ilhali yeye alikuwa ameshindwa. Hivyo kuna wengine wanaoweza kumpiku katika kupaa juu. Baada ya tukio hili, mzuka anamwambia K waende kutembea alikozaliwa ingawa K alikuwa amekusahau. Mzuka anamwambia K avue miwani yake mieusi ili aweze kuona kwao vizuri, avae figu na hatimaye ajiue ili waweze kuondoka. K anajikuta anafanya hayo yote pasi na kupenda. Baada ya K kujiua, wote wawili wanakuwa mchwa na kuingia kwenye mzizi wa ukoka.

Safari ya mzuka ya kumtembeza K inaendelea katika sura ya nane, kusudi la safari hii ni kumwonyesha K tofauti iliyoko kati ya maisha ya mjini anayoishi na ya watu waliomchagua kuwa mbunge wao. Mzuka anamweleza K kwamba 'dunia' za mji na shamba, utajiri na umaskini zimepakana na zinakimbiana. Pamoja na kutengana kwa matajiri, magari na starehe kem kem wamepakana na dunia yao jirani inayonuka (Mohamed 2001:88). Mazingira yamebadilika, misitu na vichaka vilivyokuwepo wakiwa watoto haviko, badala yake kuna jangwa na tambarare kubwa. Kijana kama Musa ambaye umri wake ni miaka thelathini hivi anaonekana kama zee la miaka sitini. Hakuna ndege au umande wa asubuhi kama siku alipokuwa mtoto. Hapo K anashtuka na kuhisi kwamba anataka ajiue yeye mwenyewe nafsi yake, mazingira yake na kwao. Anatanabahi kumbe yeye si kitu bali ni kidude kudunga, punje ya mchanga kwenye tumberare lisilo mwanzo wala mwisho. Anajiona bwege kuliko kiumbe chochote kile katika dunia hii. Sasa K anaanza kujirejesha nyuma na kwanza kujifwata na kujitafuta (Mohamed 2001:91).

Sura ya tisa inaendelea kutalii safari ya K anapokuwa akipitapita kule kijijini mwao anakumbuka alipokuwa nyumbani baada ya kupata wadhifu wake. Huu ndio wakati ambao alimnyang'anya Sururu mkewe Zuhura Mapozi wakati Sururu alipowasaidia kulikwamua limosin lake. Sururu aliwauliza waingie kwake ili wajipatie kikombe cha chai ukawa mwisho wa ndoa ya Zuhura na Sururu. Mzuka anamkumbusha K jinsi dunia yao ilivyojaa dhuluma, ingawa wezi walikuwa na haya za kuficha nyuso zao. Siku hizi za akina K bora mtu ana nguvu tu, anachukua akitakacho kwa mabavu (Mohamed 100).

Aidha K anavikumbuka vita vya wenyewe kwa wenyewe, alijifanya yuko upande wa kupigania haki lakini siku ya vita ilipofika alikwenda kujificha msituni na kuwaacha wengine akiwemo nduguye Jiba kwenda kuhatarisha maisha yao vitani; hata alipopata madaraka hakuwakumbuka. Si ajabu ndugu yake Jiba ni mmoja wa wale anaohisi wakimfuatafuata (Mohamed 2001:103).

Katika sura ya kumi na moja na kumi na mbili K anajipata nyumbani kwa Maajuzi bibi yake alikozaliwa na kukulia, aliokotwa na Jiba ndugu yake aliyejulishwa na Bi- Kali kwamba amemwona mtu aliyekuwa uchi karibu na kinu. Gromov (2002) anasema anawakilisha wananchi anapatikana akiwa anaenda kujitoka uhai baada ya kuchoshwa na maisha. K anakumbuka maisha yake ya utotoni alivyowachukia wazazi wake kwa kukubali kutimiziwa na Bw. Khalifa. Alijichukia kuwa mwana wa watumishi. Anamchukia Khalifa zaidi, kwa kuwatumikiza wazazi wake. Hata hivyo kwa upande mwingine anamhusudu. Anatamani kuwa na maisha ya kifahari sawa na ya Khalifa. Ndoto hii ya K inapotimia anasahau alikotoka na hali ya maisha ya kwao nyumbani na jamii kwa jumla.

K anaandaliwa chakula na anashangaa kuona kuwa ni togonya. Togonya ni chakula wanachokila kukiwa na njaa. Haamini kuwa nyumbani alikokulia kwa shibe siku hizi wanakula togonya, K anapomaka hivi mzuka anamkumbusha msemu wa wahehe usemao (hubede ch'lya yaani unachokidharau ndicho utakachokila siku moja. Alipokuwa mtoto alisikia chakula hiki kikitajwa kama hadithi tu.

Maneno ya maajuzi yanayoranda yale ya babu mzuka yanamkumbusha K jinsi alivyopoteza mwelekeo. Maajuzi anasema kwamba mizuka wako na wafaa kuaminiwa. Aidha K anashangaa kama watu wanakosa matibabu hadi kushonwa bila dawa za kupunguza makali kama aspirini. Anakikagua kibanda walichokuwa wakiishi na kukumbuka maisha ya kimaskini waliyoishi. Baada ya hapo, mzuka anampeleka K katika maisha ya Afrika ijayo yenye shida za kila aina na uvundo, K anapoziba pua, mzuka anamwambia asifanye hivyo bali ajiulize nani na nini sababu ya uchafu huo. Unanzia wapi na unaishia wapi. K anapelekwa mahali ambapo watu wote wanaelekea nchi za nje kuomba misaada.

Sura ya kumi na tatu K anashuhudia jinsi ufiisadi, ulivyokithiri, magari mabovu mabovu yanayokaguliwa katika kituo cha polisi kabla ya kuanza safari na pia yanapokuwa safarini. Ajabu ni kwamba baadaye magari yanakwama huko huko kwenye kituo cha polisi na inabidi lipigwe hendeli ili lingurume, linaruhusiwa kuendela na safari ingawa limeharibika. Dereva hutoa hongo kwa polisi wa trafiki ili apite. Mzuka anamwacha K anamkabidhi kwa mahakimu wakali ili wamhukumu. K anakataa kukiri hadi anakula kiapo kitiwacho kithitu. Wanamwapisha na hatimaye kumtosa baharini. Hapa ndipo sura ya kumi na nne inanzia.

K anakaa majini kwa muda huku akitapia pumzi, anafyokonyoka kutoka kitundu kidogo cha njia ya mchwa kutoka chini ya ardhi, njia aliyopitia walipokuwa na babu mzuka. Baada ya kujikaba roho K anajikuta katika dunia mnamo mwaka wa 2058 (Mohamed 2001: 148). Dunia hii ni kama jehanamu, inatisha na kuogofya. Mazingira haya yanamtia K hofu na anatemeka. Anaona dunia ikiwa mahame mabaya kuliko yale ya Pate ya Inkishafi. Hakuna barabara wala vyombo vya usafiri, watu ni wengi ingawa wote ni wakongwe. Vijana wamekimbilia nchini Uingereza na Marekani kufanya kazi ya sulubu bila hiari yao. Baadaye K anarudi kwenye ulimwengu wake anakokuta amenyang'anywa kila kitu kuanzia wafanyi kazi, magari, ofisi, mamlaka na kasri.

Sura ya kumi na tano na ya mwisho, Biye mtumishi wake K anamchukua na kumpeleka kwao kijijini. Siku mbili baadaye K anapatikana amejitia kitanzi juu ya mti uliomea juu ya kaburi la babu yake. Katika sura hii K anawatokea watoto wake Kidawa na Bamkubwa ambao siku hizi wanaishi barabarani na hali yao ni ya kusikitikiwa. Mkewe Kikuba keshakuwa mwendawazimu na yuko huko barabarani na wanawe. K kama mzuka wa babu yake anajaribu kuongea nao lakini wanakataa wakisema wafu hawafufuki. K anatembelea nchi wanayoishi akiwashawishi wajiue na kujifufua kama yeye ili waishi maisha yao ifaavyo kwa sababu yeye alikosea. Mwandishi anatumulisha kwamba watu wengi watakuwa tayari kujiua kwa maslahi ya nchi nzima na vizazi vitakavyokuja baadaye. K anakwenda kwa iliyokuwa ofisi yake kuwahamasisha waliomo wajiue na kufufuka kama alivyomwambia babu yake (Mohamed: 168).

Mtindo

Wakati: Sayansi bunilizi hujikita katika nyakati tatu, zikiwemo wakati uliopo, wakati uliopita na wakati ujao. Riwaya ya Babu Alipofufuka imeeleza matukio kwa kutumia wakati ujao na wakati uliopita. Msimulizi babu alielezea imani yao katika ufufuko katika wakati uliopita. Aidha bwana K alihimizwa na babu yake kujali hali ya kesho ya vizazi vitakavyokuja, kesho hapo inarejelea wakati ujao sifa mojawapo ya sayansi bunilizi.

Sayansi bunilizi hujikita katika hali ambapo ni muhali kubainisha kati ya hali halisi na utohalisi. Katika riwaya ya *Babu Alipofufuka* chakula cha doggy kinadaiwa kutoweka tu pindi kikiwekwa mahali pake, hali ambayo inatatanisha na kuzua hali ya jambo hilo kutoaminika. Sayansi bunilizi huhusisha matuko ya kiajabu yenye usimulizi usioaminika, riwaya ya *Babu Alipofufuka* inasheheni hali hii ambapo bwana K anakumbwa ghafla na tukio la kutibukwa na tumbo na kutokwa na harufu mbaya kinywani. Aidha kicheko kisichojulikana kinakotokea kinasikika na bwana K anashindwa kubaini iwapo hali hiyo ni ya kawaida ama alikuwa katika ndoto, vile vile hakuweza kubainisha mahali alipokuwa iwapo alikuwa duniani au ahera hili ni tukio linaloegemea sifa mojawapo ya sayansi bunilizi.

Matukio ya ajabu: Sayansi bunilizi hutumia mtindo wa kiepiki- mtindo wa safari ya masafa marefu ambayo yanaweza kuchukua muda mfupi kwa kutumia vyombo vilivyovumbuliwa na wanasayansi au kusafiri katika mawazo. Mhusika K anasafiri kwa masafa marefu pamoja na babu yake katika hali ya kuhamasishwa kuhusu historia yake na hali ya jamii.

Wahusika: Sayansi bunilizi huhusisha wahusika wa kawaida na vile vile wasio wa kawaida, wakati mwingine wahusika wa sayansi bunilizi huwa mizuka au wahusika wa kawaida, lakini waliopewa sifa zilizokithiri hali ya viumbe wa kawaida. Katika riwaya ya Babu Alipofufuka kuna mhusika babu ambaye anadaiwa kufufuka licha ya kuwa aliaga dunia muda mrefu uliopita. Kwa hivyo mhusika huyu anaegemea wahusika wa sayansi bunilizi ambao huwa na uwezo uliopita kiasi na hivyo anakuza sifa ya hali halisi na utohalisi.

Mhusika Proteus ana sifa za kibunilizi kwani anasemekana kuwa hawezi kufa lakini anaweza kujigeuza kuwa mti mkubwa; aidha anaweza kuvaa ngozi ya nyoka, ya panya au ya fisi. Mhusika huyu basi anafanya riwaya ya *Babu Alipofufuka* kuwa sayansi bunilizi kwani analeta hali ya kutobaini halisi na utohalisi. Delpiero ni mhusika ambaye alisemekana kumeza eneo zima la ardhi la pahala fulani tumboni mwake. Aidha mhusika huyu aliota mbawa na kuruka kutokomea pahala fulani na akirudi alidondosha magunia yaliyojaa unga. Huyu ni mhusika asiye wa kawaida katika dunia halisi.

Miyazawa ni mhusika ambaye alifuga kucha zenye urefu wa meli nzima na hunusa harufu kama mbwa. Binadamu halisi hawezi kumiliki sifa kama hii. Mhusika huyu pia alichimba madini kwa kucha zake. Von Heim ni mhusika mwenye uwezo wa kumfufua maiti kwa kummiminia bia kutokana na tangi lake kubwa alilokuwa akilibeba kila aendapo. Mhusika huyu pia hushiriki ushoga na kumhusisha mbwa wake katika kufanya mapenzi na wasichana wa kiafrika jambo ambalo humfurahisha sana. Mzula ambaye ni dereva wa bwana K alikuwa hajaoga kwa majuma kadha jambo ambalo si la kawaida kwa mtu ambaye ana akili taahira.

Babu anageuka kivuli na kujipenyeza ndani ya mzula dereva wake bwana 'K'. Mtu aliyesimama katikati ya barabara alikuwa amevaa chupi iliyoroa damu chapachapa. Bwana K anakumbana na wahusika ambao wanaonekana nyuso na kiwiliwili pekee na vilikuwa vinashika mapanga, viwiliwili hivi vilipasua magurudumu ya gari la bwana K. Hawa ni wahusika wasio wa kawaida. Kikundi cha watu waliokuwa wakitoboa kuta za nyumba, walipozuiliwa na walinzi waligeuka mvuke na kutoweka; hawa ni wahusika wasio wa kawaida. Wahusika wa ajabu walimhukumu bwana K kule baharini na kumlisha kiapo kwa kuwa alituhumiwa kwa kuwatesa watu wengi. Watu hawa walikuwa watano lakini hawakuonekana wala kushikika bali aliwahisi tu. Haya ni matukio ya kiajabu ambayo ni sifa mojawapo ya sayansi bunilizi. Mhusika babu aliyekufa kitambo anazungumza na bwana 'K' jambo ambalo si la kawaida kwa mtu mfu kuweza kuzungumza.

Maudhui

Usasa na Ukale: Maudhui ya usasa na ukale yanaegemea sayansi bunilizi. Sayansi bunilizi hujikita katika maudhui ya maendeleo ya sayansi na teknolojia. Maendeleo haya hukuzi ustaarabu ambapo mitindo ya ughaibuni kama kufuga wanyama pendwa huenea kote ulimwenguni na ndiposa mhusika K anaagiza jibwa lake doggy lipewe chakula. Sayansi bunilizi huhusisha maudhui ya safari za angani, Katika riwaya ya *Babu Alipofufuka* kila bwana K akilala aliota ndoto za kuruka angani.

Maudhui haya yanaegemea sayansi bunilizi kwani matukio yanayotokea hapa yanakinzana ambayo ni usasa na ukale. Mhusika K anaagiza mbwa apewe chakula ilhali kuna majirani wanaodaiwa kulala na njaa. Mhusika babu ambaye ni mzuka anakiondoa chakula pindi kiwekwapo kwani zamani mbwa walipewa chakula baada ya kila mtu kula. Usasa unapingana na ukale. Aidha bwana K anatangamana na watu ambao babu yake hakuketi nao kwani ulikuwa

mwiko na hayo yalikuwa yamepitwa na wakati. Inadaiwa kwamba bwana K akilala alikuwa akiota ndoto za kuruka angani. Mijengo na kasri la bwana 'K' lilifanana na zile ambazo huonekana kwenye sinema za filamu za sayansi ya kubuni. Aidha majengo yalikuwa sawia na yale ya enzi za baadaye yenye sura za maabara za uchunguzi wa kiatomiki na kinuklia. Uvumbuzi wa zana za kinuklia na uvumbuzi wa vyombo vya kuruka angani kama roketi ni athari za sayansi na teknolojia. Hii ni sifa mojawapo ya sayansi bunilizi.

Ustaarabu: Bwana 'K' aliishi maisha ya kistaarabu pale ambapo ana jumba la kifahari ambalo lilichorwa na bwana Baseball. Bwana K alikuwa na chombo cha kisasa alichobofya na kuwaita watu waliokuja kwa mapikipiki yaliyokuwa yakiruka angani hiki ni chombo cha kisasa kinachotokana na uvumbuzi wa sayansi na teknolojia. Aidha K anatumia kompyuta nyumbani kwake kumjuza mambo mbalimbali na uvumbuzi wa sayansi na teknolojia. Bwana K na marafiki zake wanakula chakula chenye asili ya Asia kama vile nyama za nyoka na mijusi kwa hivyo huu ni ustaarabu wa kigeni.

Kuna madai kwamba watu wa hapa nchini wanaienzi elimu ya ughaibuni kwani yao si ya maana. Bwana K anasema kuwa wanania kuboresha elimu kupitia msaada wa *British council*. Kuna klabu iliyopendekezwa na bwana Di Livio ambayo ingeitwa FKK na watakaolingia hawatakuwa wakivaa nguo bali watakuwa uchi. Kwa kuwa swala hili linaegemea maudhui ya sayansi na teknolojia ya wakati ujao basi hii ni sifa mojawapo ya sayansi bunilizi.

Utandaridhi/ utandawazi: Sayansi bunilizi hushughulikia maudhui ya athari za sayansi na teknolojia dhidi ya maadili ya jamii. Utandaridhi ni hali ambapo dunia imefanywa kuwa kama kijiji kidogo kupitia urahisishaji wa mawasiliano ya mtandao kote ulimwenguni. Nchi zilizoendelea zina uwezo mkubwa dhidi ya zile hazijaendelea kwa kuwa zimeshikilia nguzo za uzalishaji mali. Katika riwaya ya *Babu Alipofufuka* bwana K anaonekana akitumia kompyuta katika shughuli zake zote. Hata muziki anaosikiliza anafanya hivyo kwa kubofya kompyuta. Ofisi ya bwana K ilikuwa na kamera nyingi za siri kwa ajili ya kuimarisha usalama. Kamera hizi ni zao la uvumbuzi wa sayansi na teknolojia.

Aidha ofisi ya bwana K ilikuwa ghorofa ya kumi na mbili ambapo alipanda kwa kutumia lifti. Bwana K alikuwa na kaseti ya kurekodi matukio kwenye ofisi na alimwita mhazili wake kwa kubofya swichi tu. Bwana K alibadili hali kwenye ofisi yake kwa kutumia 'Air-conditioner' joto likizidi. Nyumbani kwake bwana K kulikuwa na televisheni na video zilizoonyesha filamu, vyombo hivi vyote katika riwaya ya *Babu Alipofufuka* ni zao la uvumbuzi wa sayansi na teknolojia ambayo ni sifa mojawapo ya sayansi bunilizi.

Vita vya dunia: Sayansi bunilizi husheheni vita vya dunia kwa kutumia zana za kinuklia; vita hivi ni vya wakati ujao ambavyo vilitabiriwa kupiganwa angani baada ya kuvumbuliwa kwa zana za vita. Katika riwaya ya *Babu Alipofufuka* vita vya pili vya dunia vimerejelewa pamoja na hali iliyoandamana na vita hivyo. Vita hivyo vinaweza kutabiriwa kwa kuwa sayansi bunilizi hurejelea nyakati maalum katika historia.

Dini: Sayansi bunilizi hujikita katika imani fulani, katika riwaya ya *Babu Alipofufuka* kuna maudhui ya dini ambayo yamejitokeza kupitia kwa bwana K aliyeonekana akijiandaa na kwenda msikitini kusali siku ya Ijumaa vile vile kuwa na imani katika kuwepo kwa mizuka na kufufuka kunaegemea katika dini.

SURA YA TANO

Hitimisho

Katika sura ya kwanza tulinuia kubainisha sifa za sayansi bunilizi zinazopatikana katika riwaya teule za *Bina-Adamu (2002)* na *Babu Alipofufuka (2001)*. Vile vile tulinuia kubainisha na kuweka wazi maudhui yanayoegemea sayansi bunilizi katika riwaya teule. Aidha tulikusudia kudhihirisha mbinu za kimasimulizi zinazozifanya riwaya za *Babu Alipofufuka* na *Bina-Adamu* kuwa sayansi bunilizi. Kwa hivyo, tuliangazia mada ya utafiti, usuli wa mada ya utafiti, suala la utafiti, maswala ya utafiti, malengo ya utafiti, sababu za kuchagua mada, upeo na mipaka, yaliyoandikwa kuhusu mada na nadharia ya utafiti yalibainishwa. Aidha, mbinu za utafiti ziliangaziwa zikiwepo; muundo wa utafiti, mahala pa utafiti, uteuzi wa sampuli, uchanganuzi wa data na matokeo ya utafiti yalishughulikiwa.

Katika sura ya pili tuliangazia historia ya sayansi bunilizi katika misingi ya Kimagharibi na inavyobainika katika fasihi ya Kiswahili, katika kufanya hivyo tuliweza kuangalia historia ya sayansi bunilizi katika misingi ya Kimagharibi na fasihi ya Kiswahili. Vile vile tulishughulikia historia hiyo ya sayansi bunilizi ya Kimagharibi katika vitengo mbalimbali kama vile sayansi bunilizi katika karne ya kumi na tisa ya Magharibi na Afrika, sayansi bunilizi ya mwongo wa kwanza wa karne ya ishirini katika Magharibi na Afrika, kipindi cha mafanikio makuu cha sayansi bunilizi ya karne ya kumi na tisa ya Magharibi na Afrika, sayansi bunilizi ya mwongo wa kwanza wa karne ya ishirini katika Magharibi na Afrika, kipindi cha mafanikio makuu cha sayansi bunilizi ya Magharibi na Afrika, kipindi cha kiwewe cha sayansi bunilizi katika magharibi na Afrika, kipindi cha almasi cha sayansi bunilizi katika magharibi na Afrika, kipindi cha mwamko mpya cha sayansi bunilizi katika Magharibi na Afrika, kipindi cha wanawake katika sayansi bunilizi, kipindi cha kukomaa kwa filamu za sayansi bunilizi na kipindi cha milenia mpya cha sayansi bunilizi.

Katika sura ya tatu tuliangazia riwaya ya *Bina-Adamu* kama sayansi bunilizi. Pia tuliangazia historia fupi ya uandishi wa K. W. Wamitila, muhtasari wa riwaya ya *Bina-Adamu*. Aidha tuliangalia vipengele vya mtindo, wahusika, wakati na maudhui katika kubainisha na kuweka

wazi sifa za sayansi bunilizi zinazopatikana katika riwaya ya *Bina- Adamu*. Na katika sura ya nne tuliangazia sayansi bunilizi katika riwaya ya *Babu Alipofufuka* ambapo tuliangazia historia fupi ya mwandishi Said Ahmed Mohamed, muhtasari wa riwaya ya *Babu Alipofufuka* na vile vile tukashughulikia mtindo, wakati, matukio ya ajabu, wahusika na maudhui katika kubainisha na kuweka wazi sifa za sayansi bunilizi zinazopatikana katika riwaya ya *Babu- Alipofufuka*.

Mchango

Utafiti huu umechangia kuonyesha kwamba sanaa ya sayansi bunilizi ipo katika fasihi ya Kiswahili na ilikuwa haijafanyiwa utafiti wa kina. Kazi hii ni miongoni mwa tahakiki za kwanza kufanywa kuhusu sayansi bunilizi katika lugha ya Kiswahili.

Fasihi ya Ubunilizi wa Kisayansi ni kioo cha jamii kinachoonyesha maendeleo ya kiteknolojia katika jamii zetu. Kutokana na utafiti huu, maendeleo ya kiteknolojia yanaathiri jamii zote hata zile zinazotumia lugha ya Kiswahili. Juu ya hayo utafiti huu umechangia katika kupanua lugha ya Kiswahili kwa kuwa dhana mbalimbali zilibunniwa kama vile ubunilizi wa kisayansi, nadharia ya kibunilizi, ukweli wa kibunilizi miongoni mwa zingine katika utafiti huu. Kuna baadhi ya maneno mapya yaliyotumiwa katika riwaya ya *Babu Alipofufuka* na *Bina Adamu* kama vile: Bina, bini, deki masen, fyura, gastarbeiter, kenya, mwega, shiraa, vitas, topedo, mnyotoo, lailalati-kadir, nauka, thomu miongoni mwa maneno mengine. Maneno haya yanaweza kutoholewa na kujumulishwa miongoni mwa istilahi za lugha ya Kiswahili. Jambo hili linabainisha kuwa sayansi bunilizi ni kipera cha fasihi ya Kiswahili na kinaweza kujumulishwa katika fasihi ya Kiswahili na kufundishwa katika vitengo vya shule za upili na vyuo vikuu. Hivyo basi lugha ya Kiswahili imekuzwa kwa kiasi fulani kupitia utafiti huu.

MAREJELEO

Aldiss, B. (1973), *Billion Year Spree: The True History of Science Fiction*. New York; Schocken Books.

Anaye, J.V. (2014), *Hadithi Kama Chombo cha Maudhui Katika Fasihi Uchanganuzi wa Riwaya za Mkangi G. K. Mafuta (1984) na Walenisi (1995)*. Tasnifu za Uzamili (M.A) Chuo Kikuu Cha Kenyatta.

Asimov, I. (1955), *The End of Eternity*. Greenwich: C.T. Fawcett Crest.

Ballard, J.G. (1962), *The Drowned World*. New York: Berkley Publishing Corporation.

Bell, W. (1997), *Foundations of Future Studies: Human Science for a New Era*. New Brunswick: Transactions Publishers vol II.

Bester, A. (1953), *The Demolished Man*. New York: Signet.

- Bova, B. (Ed.) (1973), *The Science of Fiction. Hall of Fame. Vol IIB*. New York: Avon Books.
- Clarke, A. C. (2001), *A Space Odyssey*. New York: Ballantine Books.
- Clute, J. (1995), *Science Fiction: The Illustrated Encyclopedia*. London: Dorling Kindersley.
ISBN
- Cooper, D. (Editor) (1995), *A Companion to Aesthetics*. U.S.A. Blackwell Publishing Ltd
- Crispin, E. (1968), *The Stars and Under: A Selection of Science Fiction*. Great Britain: Faber & L.T.D.
- Dietrich, R. F. et al (1965), *The Art of Fiction*, New York; Holt Rinehart and Winston Inc
- Disch, T. (1998), *The Dreams Our Stuff is Made of: How Science Fiction Conquered The World*.
New York: The Free Press.
- Fast, H. (1959) *The First Men "in The Edge of Tomorrow"*. New York: Bantam Books.
- Frank, A. T. and Steven, M. C. (1969), *Philosophy of Art and Aesthetics, From Plato to Wittgenstein*, New York: Harper and Row.
- Heinlein, R. (1967), *The Past through Tomorrow*. New York: Berkeley Publishing Corporation.
- Hoskins, R. (1972), *Wonder Makers: An Anthology of Classic Science Fiction*. Greenwich:
Fawcett Publications inc.
- Howard, F (1999), (E.d) *Frontiers of the 21st Century: Prelude to the New Millennium*.
Bethesda, Maryland: World Future society.
- Kennedy, X. J. & Dana, G. (2003), *Literature: An Intrdocution to Fiction, Poetry and Drama*,
Third Edition U.S.A: Longman.
- Mark, P. (editor) (1980), *Reference, Truth and Reality*, London : Routledge and Kegan Paul.
- Mchale, B. (1992), *Constructing Postmodrnism*; London, Routledge.
- Mkangi, K. (2003), *Walenisi*. Nairobi: E.A.E. P.
- Mohamed, S. A (1988), *Pungwa*. Nairobi: Longhorn Publishers.
- _____ (2001), *Babu Alipofufuka*, Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- _____ (2006), *Posa za Bi Kisiwa*. Nairobi: Sasa Sema Publications.

- _____ (2006), *Dunia Yao*. Nairobi: Sasa Sema Publications.
- Mohamed, S.A na King'ei K. (2006), *Posa za Bi Kisiwa*. Nairobi: Sasa Sema Publications.
- _____ (2011), *Janga La Werevu*, Nairobi : Sasa Sema Publications.
- _____ (2013), *Mkama Ndume*, Nairobi: Longhorn Publishers.
- Newell, S. (2002), *Readings in African Popular Fiction*. Bloomington ; Indiana University Press.
- Njogu, K. S. na Chimerah. (1999), *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- O'connor D. J. *The Correspondence Theory of Truth*, London: Hutchnson & Co.
- Odyssey, (1988), *Three*: New York: Ballantine Books.
- Orwell, G. (1949), *1984*. New York: Hartcourt, Brace and company.
- Peter, C. (2000), *Reading Fiction: Opening the Test*, Great Britain: Creative Print and Design Wells.
- Robert, S. (1967), *Kufikirika*. London : Nelson.
- _____ (1951), *Kusadikika*. London : Nelson.
- Thomas, I. (2006), *The Evolution of Future Consciousness*. Bloomington Indiana: Author House.
- TUKI, (1996), *English-Swahili Dictionary*. Dar-Es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.
- _____ (2004), *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*: Dar es Salaam: TUKI.
- Vinge, V. A (1992), *Fire Upon The Deep*. New York: Tom Doherty Associates.
- Wachhorst, W. (2000), *The Dream of Spaceflight: Essays on the Near Edge of Infinity*. New York: Basic Books.
- Walibora, K. W. (2010), *Swahili Forum* 17 (143-157).
- Wamitila, K. W. (2002), *Bina Adamu*. Nairobi: Phoenix Publishers.
- Wamitila, K. W. (2003), *Kamusi ya Fasihi Istilahi na Nadharia*, Nairobi: Focus Books.
- _____ (2012), *Harufu Ya Mapera*. Nairobi: Vide Muwa.
- _____ (2012), *Mikakati Ya Uhalisiajabu katika riwaya ya Kiswahili.Mulika*.

_____ (2013), *Tikiti Maji*. Nairobi: Vide Muwa.

Wells, H. G. (1973), *Seven Science Fiction Novels of H.G. Wells* New York: Dover publications Inc.

<http://www.worldcon.org/hy.html>.- The Hugo Winners- Science Fiction

<http://www.depauw.edu/sfs/backissues/78/hollinger78art.htm>

<http://www.odysseyofthefuture.net/listing/readingspaceexploration.pdf>.

<http://www.sfwa.org/awards> The Nebula Winners-Science Fiction and Fantasy Writer of America inc

<http://www.treitel.org/richard/sf/sf.html>.defition of science fiction